

# Sera Ya Haki Ya Kijinsia

THE LUTHERAN WORLD FEDERATION

A Communion of Churches

# Yaliyomo

Dibaji.....................................................................1

Kutembea pamoja kwenye barabara ya haki ya jinsia: Safari ya Kiufundishaji..........................................................2

Msingi wa kibiblia na sababu za msingi..............................4

Kanuni za haki ya kijinsia ya LWF......................................13

Mbinu ya haki za kijinsia ya LWF.......... ..........................14

Faharasa.....................................................................37

Nyenzo zaidi za sera ya kijinsia kwenye mtandao................40

Mhariri: Elaine Neuenfeldt

Ubunifu na Mpangilio: Huduma ya Mawasiliano

Idara ya Theolojia na Ushahidi wa Umma

Picha: © Barbara Robra na © Shirikisho la MaKanisa ya Kilutheri Duniani

Mchapishaji: The Lutheran World Federation – Ushirika wa MaKanisa

Idara ya Theolojia na
Ushahidi wa Umma
Wanawake katika
Kanisa na Jamii
Route de Ferney 150
P. O. Box 2100
1211 Geneva 2,
Switzerland
Imechapishwa Uswisi
ISBN 978-2-940459-31-5
info@lutheranworld.org

## Dibaji

Wito wa Biblia wa kutetea haki uko moyoni na katika ufahamu wa Jumuiya ya LWF. Neema ya Mungu hutukomboa, hutuleta pamoja na Kristo na hutuwezesha kuishi na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya haki, amani na upatanisho.

LWF imejizatiti kuwa pamoja na kuwezesha ushiriki kikamilifu wa usawa wa wanawake na wanaume katika maisha ya Kanisa na jamii, na katika mchakato wake wa kimaamuzi, shughuli na mipango yake. Inaangalia nyuma kwenye historia ya maamuzi na vitendo vinavyoonyesha jinsi ilivyojikita katika hili.

Sera hii ya Haki ya Kijinsia ya LWF, iliyopitishwa na baraza la LWF mwaka 2013 ni chombo cha kufanikisha mpango wa kujumuika pamoja. Sera hii iliyoandaliwa kwa mchakato shirikishi imetokana na uzoefu wa makanisa wanachama na ilistawishwa katika misingi ya Kibiblia na kitheologia ya utambulisho wetu wa Kilutheri. Hutoa mwongozo na mbinu kwa ajili ya kuweka mpango kazi katika mtazamo na mikakati katika kanda na kufungamanisha jinsia kama kipaumbele kinachoibuka katika kazi zote za umoja/ushirika.



Katibu mkuu wa LWF Mchg. Martin Junge

© LWF/H. Putsman-Penet

Kama ilivyo historia ya LWF ya kujitoa kuondoa ukatili dhidi ya wanawake na hali yake ya kuwakubali wanawake katika nafasi za uongozi, sera ya haki ya jinsia ni tukio lingine muhimu tena wakati LWF inasonga kuelekea taswira yake ya ujumuisho utaratibu uliendelea katika waraka huu umefungua madirisha ya fursa ya kujihusisha katika vuguvugu za kubadilika katika mahusiano na miundo. Ni mwaliko wa kila mmoja hasa viongozi wa Kanisa, watheolojia wanawake na wanaume walioko katika uongozi na kwenye nafasi za kufanya maamuzi, watu wanaosimamia mipango na miradi – kukubali haki ya kijinsia kama jambo la kiimani. Hivyo, haki ya kijinsia huonyeshwa kwenye mipaka ya misingi ya uwepo wa Kanisa na sauti yake ya kinabii katika umma.

Sera ya haki ya kijisia imekuja wakati ambapo wanawake wanaendelea kukabilianana na changamoto katika Kanisa na jamii. Wanawake na wanaume wanaendelea kusikia wito wa Mungu kuhusu mahusiano yenye msingi katika haki. Kimechapishwa nyakati ambazo jumuiya ya LWF inapata kusikia wito wa uhuisho endelevu (semper reformanda) inapojiandaa kwa ajili ya sikukuu ya miaka 500 ya matengenezo ya Kilutheri mwaka 2017. Nakabidhi

kwa ajili ya mafunzo yaambatanayo na maombi ili hekima ipate njia/au namna ya kudhihirishwa katika miundo na maisha ya Kanisa kwa ujumla.

Kwa sababu mahusiano ya kijinsia yako chini ya nguvu ya Mungu ibadilishayo wataweza kubadilishwa/kuhuishwa ili wawe wa haki na usawa.

Rev. Martin Junge

Katibu mkuu

Fungamano la Makanisa ya kilutheri Duniani.



# Kutembea Pamoja Katika Njia ya Haki ya Kijinsia: Safari ya Kiufundishaji

> Jiwekee alama za njia; jifanyie miti ya kukuongoza: uelekeze moyo wako kwenye njia kuu, njia ile ile uliyoiendea. (Yer 31:21).

Katika umoja wa LWF, mjadala wa kiufundishaji juu ya haki ya jinsia uchangiaji katika tafakari pana kuhusu jinsi tunavyokusudia kufundisha, kujifunza, kusindikizana, kuonyana na kuendelea kusaidiana sisi kwa sisi tunapoendelea kusafiri pamoja kulekea kwenye umoja ambao ujumuisho unadhihirishwa katika maisha.

Sera ya haki ya jinsia ya LWF imetulia kwenye masharti na kanuni yanayoelekeza hatua dhabiti kuelekea utekelezaji wa haki ya kijinsia. Hili hufanikisha mchakato wa kuchukua mpango kazi katika uhalisia wa mtazamo tofauti.

Hivyo tunasoma,

sheria ya Bwana ni kamilifu

huiburudisha nafsi ushuhuda

wa Bwana ni amini humtia

mjinga hekima, maagizo ya

Bwana ni adili huufurahisha

moyo, amani ya Bwana ni safi

huyatia macho nuru, kicho

cha Bwana ni kitakatifu

zinadumu milele, hukumu za

Bwana ni kweli zina haki

kabisa, ni za kutumainika

kuliko dhahabu, kuliko wingi

wa dhahabu safi, nazo ni

tamu kuliko asali kuliko sega

la asili (Zab 19:7–10).

Picha ya kibiblia ya masharti na kanuni hufufua roho na kufurahisha moyo huwasaidia wanawake na wanaume kuumba tena haki na hadhi katika uhusiano.

Waraka umegawinyika katika sehemu mbili, kanuni ya sera ya haki ya kijinsia na mbinu ya sera ya haki ya kijinsia. Kanuni ya sera ya haki ya kijinsia ya LWF inatoa mwongozo wa kuelekeza utumikaji wa haki ya kijinsia kwa kujitoa katika ngazi zote za ushirikiano.

## Kanuni ya Sera ya Haki ya Kijinsia

Kanuni kumi ni msingi katika kuelezea ukubali wa ushirikiano wa LWF kuhusiana na haki ya kijinsia. Ni kiini cha kuonyesha nini maana ya haki ya kijinsia kwa ushirikiano, ni vioo ambavyo vitendo vya ushrikiano vitachunguzwa na kama ishara, vibao au ishara za barabarani kuelekea safari ya haki ya kijinsia ya ushirikiano.

## Mbinu ya Sera ya Haki ya Kijinsia

Mbinu ya sera ya haki ya kijinsia hutoa zana za utekelezaji wa kanuni ya haki za kijinsia kupitia udhihirisho wa kikanda na Makanisa wanachama kwa matarajio kuwa itachukuliwa na Makanisani yote.

Mchakato utakuwa ukisimamiwa kupitia majukwaa ya kikanda yaliyounganishwa na udhihirisho wa kikanda. Katika ngazi ya kiulimwengu, katibu mkuu atataarifu maendeleo ya utekelezaji wa sera ya kijinsia ya LWF katika ushirikiano katika taarifa yake kwa baraza.

Mbinu na vifaa vitaendelezwa ili kwamba mipango na michakato zimilikiwe na kufikiwa na makundi husika katika Makanisa wanachama.

Kusudi ni kuanzisha mduara wa kujifunzia na jumuiya za utendaji ambapo ujuzi unashirikishwa na kusaidiana pande zote kwa manufaa ya pamoja na kufanya kwa ufanisi.

# Misingi na Sababu za Kibiblia

Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na dunia, nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji… Mungu kaona kila kitu alichokifanya, natazama, ni chema sana. (Mw 1:1-2, 31a).

Katika kitabu cha Mwanzo, hadithi ya uumbaji inaonyesha kwamba vitu vyote vilivyoishi ni kwa kumtegemea Mungu. Hadithi ya uumbaji katika kitabu cha Mwanzo 2 hutumika huhoji kuwa si tu kwamba wanadamu wametofautiana; bali pia kuwa aina moja ya wanadamu (mwanaume) ni bora kwa mwingine (mwanamke). Hata hivyo hadithi za uumbaji katika mwanzo zaweza pia kueleweka kuwa inaonyesha wazo la kuwepo tofauti muhimu sana iliyopo baina ya Mungu na uumbaji, sio kati ya mwanaume na mwanamke. Uumbaji humtegemea Mungu. Huu ni uhusiano wa msingi wa kitheologia na kuhusu uumbaji.

Utofauti huu wa msingi kati ya Mungu na uumbaji unafafanuliwa kwa upendo sio kwa ubaguzi wa kijinsia ndani ya au kati ya wanadamu. Hata kama hadithi ya uumbaji mara nyingi inasomwa kwa kuegemezwa sio tu utofautishaji wa jinsia bali pia kudhalilisha wanawake ukifananisha na wanaume,uchambuzi wa maandiko zaidi yanaonyesha kuwa hivi sivyo.

Kipengele kingine cha kuanzia ni usawa (ling. Mw. I:27). Mungu alimuumba kila mtu kwa usawa. Mungu pia anawaita wanadamu kwa usawa katika wito wa kushirikiana wa uwakili wa kutunza uumbaji wa Mungu unaoendelea.

Maadili ya kutunza na kupenda hujumuishwa katika maandiko haya ya kitabu cha Mwanzo hukaza adili ya haki ya kijinsia kwa sababu ukarimu, upendo na ujumuisho wa tofauti hudumu katika mtazamo kuwa mara nyingi watu wako mbele ya macho au uwepo wa Mungu. Wanadamu kwa pamoja wanaitwa kuwa mawakili kila moja kwa mwenzake na kwa uumbaji mzima.

Kisha Mungu akasema “na tumfanye mtu kwa mfano wetu na kwa sura yetu: wakawatawale samaki wa bahirini, na ndege wa

> angani, na wanyama wote wa nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi" Mungu akaumba mtu kwa mfano wake , kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba (Mw 1:26-27).

Roho Mtakatifu anatoa msingi wa ujumuisho, kama tusomavyo katika injili, namna ambavyo Yesu alivyohusiana na wanawake kulivyo wazi, kujumuisha ya ukaribisho na ulinganisho. Shuhuda za kibiblia zinakubali kuwa neno la Mungu ni neno la uzima kwa wote wanawake na wanaume.

Kama jumuiya ya usawa, kupita ubatizo, Kanisa liliitwa la kinabii kwa kutangaza na kudhihirisha ujumuisho. Kama tusomavyo katika Gal (3:27-28).

> Kama wengie wenu mlivyobatizwa katika Kristo mlimvaa Kristo pamoja nanyi. Hamna tena myahudi wala mgiriki, hamna tena mfungwa wala aliye huru, hamna tena mtu mke au mtu mume, kwa kuwa wote mmekuwa mmoja katika Kristo.

Kwa ajili ya uhusiano wa kijinsia, maandiko haya kibibilia na kithiolojia huhimiza umoja, kuwa katika jumuia, katika mjadala unaobadilisha. Ushiriki mkamilifu na ulio sawa wa wanaume na wanawake unawezekana pale ambapo mipaka ya ubaguzi wa kijinsia inapovunjika, kwamba wale walio chini hasa wanawake na wanaume pia wamevunja maadili na hadhi yao waliopewa na Mungu. Ushirikiano unapoendelea katika safari yake ya imani na matumaini, Roho Mtakatifu hutuweka huru kutafsiri maandiko ya bibilia katika namna ya kuhuisha na kuimarisha maisha. Huu ni msingi unaotoa mamlaka ya kivitendo ambao unachukuliwa katika ngazi ya maamuzi katika LWF.

## Mamlaka

Mnamo oktoba 2009 baraza la LWF lilipokea waraka na *"Lakini haitakuwa*

*hivyo kwenu*" *Mtazamo Wa Imani Katika Jinsia Na Mamlaka*[1] na kupigiwa kura "ili kuwatia washiriki wa Makanisa kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufuatiliaji unaoleta maendeleo katika sera ya jinsia ya LWF."

Mnamo mwaka 2010, mkutano mkuu wa kumi na moja LWF ulifikia maamuzi muhimu yafuatayo:

**Kanuni ya LWF ya ujumuisho:**
***Uwiano wa kijinsia:***



[1]Inapatikana
**www.lutheranworld.org/content/resource-%E2%80%9Cit-will-notbe-so-among-you%E2%80%9Dfaith-reflection-gender-and-power**

Mkutano mkuu w LWF, baraza, maafisa, na kamati zingine zote na vikundi kazi, pamoja na ngazi za kikanda vyote vitajumuisha angalau asilimia 40 ya wanawake na angalau asilimia 40 ya wanaume. Kwa njia hiyo usawa wa kijinsia utakuwa umeheshimiwa pia kati ya uwakilishi wa vijana.

Katika shughuli zote ambazo huongozwa, katika ngazi zote za kikanda, LWF itaheshimu kanuni hii ya msingi, na wafanyakazi wa LWF watawatia moyo na wale ambao wanafanya kazi nao pia[2]. Kanuni ya msingi inatumika kwa wafanya kazi wa LWF katika ofisi ya makao makuu ya ushirikiano[3].

[2] Acknowledging the existing challenges, meetings and activities in which the basic principle has not been applied are not to be declared invalid, but their non-compliance with the basic principle shall be formally recognized and actions to improve on this need to be planned.

[3] *Give Us Today Our Daily Bread*, Official Report, LWF Eleventh Assembly, Stuttgart, Germany, 20–27 July 2010 (Geneva: The Lutheran World Federation, 2010), 61.

### Maazimio kuhusu haki ya kijinsia:

Tunaita Umoja ili kuwataka washirika wa Kanisa kujitoa tena katika utekelezaji wa sera za LWF na maamuzi yanayohusiana na ushiriki kikamilifu wa wanawake katika mambo yote ya maisha ya Kanisa- na ushirika wa LWF – na jamii kwa ujumla.

Tunawataka washiriki wa Kanisa kuweka sheria sahihi na sera za kisheria zinazowawezesha wanawake kushiriki katika nafasi za uongozi – wasimikwe – na wapewe fursa ya kusoma masomo ya kitheolojia tunawaomba Makanisa ambao hawa wasimiki wanawake tuwaombe watafakari madhara yatokanayo na kukataa kwao kuwasimika – wito wao waliopewa na Mungu kwa sababu tu ni wanawake. Maumivu ya kutengwa pamoja na kupoteza vipawa walivyopewa na mwenyezi Mungu yanapitiwa na Kanisa zima.

Tunawataka washirika wa Makanisa yote na sekretarieti ya LWF wajumuishe uchambuzi wa kijinsia kama zana ya kibibilia na ya kitheolojia katika maeneo yote ya maisha ya washiriki wa Kanisa katika ushirikiano pamoja na kazi za kidiakonia na utetezi.

Tunawaomba mpango kazi ulio wazi kwa ajili ya kuendeleza sera ya kijinsia inayojali mukutadha ambayo inaweza kutekelezwa katika ngazi zote na Makanisa wanachama na iwe lazima pia kwa sekretarieti ya LWF tunataka baraza liendeleze

na kuthibitisha miongozo hiyo ya mchakato.

Tunahitaji msaada wa wanawake viongozi, walei na walio simikwa, hasa wanawake, maaskofu na marais, kama washiriki muhimu kwenye ushirika.

Tunataka LWF na Makanisa washirika waweke msimamo wa wazi dhidi ya unyanyasaji wa nyumbani, watambue haki ya kila mtu kujisikia salama na kuhudumiwa kwa heshima, hata wakiwa nyumbani mwao.

Tunaliomba baraza wawe na suala la haki ya kijinsia kama agenda inayojitegemea. Kwa sababu kuna uwiano kati ya vijana wa kiume na wakike katika baraza, baraza lazima liangalie hili kipekee[4]

Mikutano ya mwaka 2012 huko Bogota, Kolombia, baraza la LWF liliomba ushirikiano ofisi ya kuwakilisha nakala ya LWF ya sera ya haki ya kijinsia katika baraza 2013. Sera ya kijinsia ya LWF ilichukuliwa na mkutano wa baraza huko Geneva juni mwaka 2013.

[4] Ibid., 56.

## Ufafanuzi

Sera ya kijinsia ya LWF huonyesha baadhi ya kanuni na kutoa msingi wa ushirikiano kufikia haki ya kijinsia.

**Haki ya kijinsia** inaonyesha uhifadhi na utunzaji wa hadhi ya mwanamke na mwanaume ambao aliumbwa kwa mfano wa Mungu na ni mawakili



wawajibikaji juu ya uumbaji wa Mungu, haki ya kijinsia huonyeshwa kupitia usawa na uwiano wa uongozi katika uhusiano kati ya wanaume na wanawake na uondoaji wa taasisi, na mifumo ya kiutamaduni na ubinafsi inayoleta manufaa na uonevu unaoendekeza ubaguzi.

## Haki ya kijinsia: Maono ya ushirika

Kuokolewa kwa neema ya Mungu ushirikiano katika Kristo unaoishi na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya ulimwengu wa haki, amani na upatanisho[5]

[5] *LWF Strategy 2012–2017*, 9, at **www.lutheranworld.org/content/core-lwf-documents**

Ushirika umeitwa kuishi na kufanya kazi na Kristo kusemea unyanyasaji na uonevu na kutengeneza ukweli unaobadilisha jamii yenye maisha mazuri na uhusiano wa haki ya kijinsia inayolea na kuongoza ushamiri wa wanadamu.

Kuwa katika ushirika humaanisha kushirikiana katika safari ya kiroho, kulelewa na injili ya neema ya Mungu na kupokea na kuishi ndani ya ubatizo na kushiriki pamoja katika ushirika mtakatifu wa Mungu na kwa kila mmoja. Kuwa katika Kristo humaanisha ingawa tofauti zetu zinabaki, zina maana tofauti: tofauti zetu ni vipawa – hakuna aliye bora kuliko mwenzake. Tofauti hazipelekei kupotea kwa usawa.

Mtazamo wa jinsia ni kuhusiana na kuchangamana na makundi mengine ya kijamii. Mtazamo wa mgawanyiko kudhani kwamba vipengele fulani vya utambulisho ni vyanzo vya ubaguzi vinavyohusiana na kila mmoja: vipengele hivyo kama vile jinsia, jamii, vikundi, umri, ulemavu, na madaraja vinahusiana katika ngazi ya mtu binafsi na ya taasisi. Kuna mifumo ya kutowiana: hii huhitaji kuchambuliwa tofauti ingawa zimeungamanishwa katika ncha ya ukandamizaji. Zana zingine pia ni msaada katika kusemea ukweli wa uonevu kulingana na kabila, madaraja na umri, na viko katika kuchangamana na mambo ya kijinsia ambavyo taasisi inaweza ikachukua hatua zitakazopelekea mabadiliko.

Uhusiano wa kibinadamu pamoja na miundo hufanikishwa na mifumo na taasisi ambayo huhakikisha kuwa haki inatendeka. Taasisi za kimataifa na kiulimwengu kama vile umoja wa mataifa, (UN) hutoa muongozo wa usawa wa kisheria kuongoza nchi na vikundi binafsi. Haki katika vitendo inatambuliwa katika sera hii ya haki ya kijinsia ya LWF. Kati ya taasisi za kidini (FBOs) na Makanisa dhana ya haki inachangamana na uelewa wa

kitheologia na kibibilia. Haki inazungumzwa katika bibilia, lugha za kitheologia na kinabii. Uelewa huu hutoa mtazamo wa undani katika mtazamo na hukusudia kuchambua ukweli na zana ambazo ziko katika mjadala na mtazamo wa haki za binadamu na dhana za kitheologia.

Uendelezaji wa sera ya haki ya kijinsia ya LWF, kanuni na mbinu ni juhudi za kukamilisha hali ya kujitoa hapo juu katika eneo la haki ya kijinsia na kuwawezesha wanawake na wanaume kuhakikisha uchambuzi wa jinsia katika shughuli na miundo yote.

Kigezo: tunapoweka vigezo vya haki ya kijinsia, swali moja la msingi ambalo linahitaji kuibuliwa ni, watu waliotengwa na kubaguliwa dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia wanahitaji nini?

Baadhi ya vigezo vilivyoorodheshwa hapo chini vinaweza vikatumika kama viashiria vya kawaida kupima mabadiliko ya jumla katika tabia au muundo wa taasisi kuhusiana na haki ya kijinsia.

- Mtazamo usio na madhara: unyanyasaji wowote, hupoteza maisha au uwezo – kama unavyofafanuliwa na kikundi pasipo manufaa ya kijamii au ya kidini
- Viashiria vya maelezo: ushiriki wa usawa wa wanawake na wanaume (katika tarakimu): uhusiano wa ushiriki (ubora)
- Ushiriki sawa: katika uongozi na kufanya maamuzi – ubora na wingi
- Uwiano katika kufikia: kufikia na kutumia rasilimali
- Kutumia: maandiko ya umoja wa mataifa na viwango vya umoja wa mataifa vya haki za bianadamu kisheria.

Katika kila mtazamo viashiria fulani vithibitisho, idadi, maoni au mtazamo lazima uelezewe kuonyesha mabadiliko au maendeleo katika kutilia mkazo mipango kazi kwa ajili ya utekelezaji wa kanuni ya haki ya kijinsia kama ulivyoorodheshwa katika sera hii.

## Lengo

Sera ya haki ya jinsia ya LWF kutafuta, kutoa ridhaa ya kisiasa na zana ambayo huchangia katika kufanikisha haki ya kijinsia ili kufikia ujumuisho endelevu kwa jamii na Makanisa.

Sera ya haki ya kijinsia ya LWF ni kutumika kama chombo kwa ushirikiano na Makanisa wanachama wake, Makanisa, vikundi na taasisi ili kufikia usawa wa kijinsia kwa kutekeleza hatua za mtazamo zinazo kuza haki na hadhi.

## Kusudi: kwanini sera ya haki ya kijinsia?

Kusudi ni kutengeneza misukumo ya ubunifu ambayo huchangia kwa mfano mabadiliko ya kijamii katika hali, desturi thamani au uhusiano wa

uongozi pamoja na mikakati mingine ambayo husaidia kuhakikisha haki ya kijinsia. Inatarajiwa kuwa kutumika kwa sera ya haki ya kijinsia ya LWF itaongoza Makanisa wanachama na ofisi ya ushirikiano kufanya yafuatayo:

- Kutambua ni sera na miongozo yake kwa utekelezaji kama hali ya kujitoa ya ushirika kwa ajili ya haki ya kijinsia.
- Kujihusisha katika tathmini shirikishi ya rasilimali ya changamoto kwa Kanisa wanavyoendelea kuelekea kufikia kwenye haki ya kijinsia.
- Uchambuzi ushiriki wa wanawake na wanaume katika maisha ya Kanisa katika masuala ya uwepo wao katika ngazi za maamuzi na kufikia kwao elimu ya kitheologia na kusemea unyanyasaji katika eneo hili.
- Kutia moyo wanaume na wanawake wajadili na kutafakari kwa kuangalia wajibu ambao wamekuwa wakijihusisha nao kiutamaduni, kusogea zaidi ya majukumu waliopewa kiutamaduni na kimila katika maisha ya Kanisa na jamii ili wale wenye ujuzi wa kutumika katika maeneo mengine waboreshe utambuzi katika Kanisa na jamii.
- Kutia moyo uongozi wa Kanisa kujadili na kutafakari juu ya ufafanuzi wa maandiko matakatifu ambayo huangazia mwanga tofauti kuhusu maana ya andiko na kama ni lazima, ufafanuzi mpya utolewe kurejea majukumu na wajibu wa wanawake na wanaume. Viongozi wa Kanisa wanayo fursa kufanya kazi na viongozi wakidini na wa kidunia ili kuunga mkono usawa wa kijinsia.

### Sera ya LWF ni nini?

Sera ni udhihirisho wa thamani, taswira inayotoa maelekezo na muongozo wa kufanikisha usawa wa kijinsia. Hutoa mwongozo wa makusudi. Kuna hatua tofauti za ushiriki wa kisiasa katika ushirikiano. Kwa mujibu wa Makanisa wanachama ushirikiano una mfumo kwa namna ambavyo mabaraza na mikutano ya maamuzi yamejikita katika uambatanishaji na uwajibikaji. Katiba hueleza wazi kuwa LWF ni chombo cha Makanisa washirika huru na haina mamlaka yoyote ya kiurasimu.

Pamoja na uhuru majukumu huja pia kwa hicho Kipengele cha III cha katiba, asili na kazi hueleza kuwa Makanisa washirika "yanakubaliana katika kutangaza neno la Mungu na yameunganishwa katika ushirika wa altari na mimbari". Zaidi pia, LWF,

zaidi ushuhuda wa ushirika katika kristu ….. Kuendeleza mikakati ya diakonia katika maKanisa washirika kushughulikia mahitaji ya kibinadamu kukuza amani na haki za kibinadamu, haki za kiuchumi na ki jamii, kutunza uumbaji wa Mungu na kushirikiana rasilimali: Kuendeleza kupitia ushirikiano masomo ya

kujitambua na ushirika wa maKanisa wanachama [6]

Kwa hiyo sera ni njia moja wapo ambayo LWF huonyesha ushuhuda wa muunganiko wa Makanisa wanachama kukuza haki za binadamu na kujielewa. Ni njia moja wapo ya kuelezea kwa undani zaidi nini maana ya kuwa katika ushirikiano katika ngazi tofauti au maeneo tofauti ya majukumu.

## Maazimio ya Baraza

Katika mkutano wake wa baraza la mwaka 2013 fungamano lilipiga kura

kuchukua sera ya haki ya jinsia ya LWF (kanuni na mapendekezo yake kama mwongozo wa utekelezaji wa haki ya jinsia katika kujitoa kwa ngazi zote za ushirika;

Kupokea mbinu ya sera ya haki ya kijinsia ya LWF na kupendekeza utekelezaji wake kupitia maelekezo ya kikanda na Makanisa wanachama kwa matarajio kuwa mbinu itabadilishwa hadi ngazi za chini:

Kumuomba Katibu Mkuu kutoa taarifa kwa baraza juu ya maendeleo ya utekelezaji wa Sera Ya Kijinsia ya LWF katika ushirika. [6]

## Ngazi za majukumu

Pamoja na katiba ya LWF hatua zifuatazo zinahusika katika utekelezaji wa sera:

### Fungamano la baraza na mikutano ya maafisa wote

- Watatumia sera kutoa mwongozo wa jumla na kupanga kazi katika ofisi ya ushirikiano: bodi ya uongozi wanawajibika kuhusu kuchambua na kuonyesha sera na maamumuzi kwa wanawake na wanaume na kuhakikisha kuwa muundo wa taasisi na mipango kazi vinaendana na kanuni ya haki ya kijinsia.

[6] inapatikana **www.lutheranworld.org/content/core-lwf-documents**

### Ofisi ya ushirikiano, mipango na miradi yake, pamoja na mipango ya LWF katika nchi

- Wanapaswa iwezekanavyo kutekeleza sera kuendeleza na kutathimini kazi. Kutekeleza sera kazini pamoja na kujitoa kuongeza ufahamu na ujuzi, kutoa vielelezo na mfumo wa uwezeshaji inayopelekea haki ya kijinsia. Utawala unapaswa kufanya mapitio mathubuti ya mifumo ya taasisi na kujitoa kwa ajili ya uchambuzi wa jinsia, na kuhakikisha kuwa mifumo na vigezo vya kutosha vimeandaliwa ili kuendeleza usawa wa kijinsia na haki katika mipango kazi na wafanya kazi wake.

## Washarika

- Kuhakikisha utekelezaji wa maamuzi na maazimio katika ngazi za fungamano na baraza na kuunga mkono na kushirikiana kila mmoja katika kuchunguza ufuatiliaji wa kina wa sera ya kijinsia katika uwajibikaji wenye tija.

Uhuru wa kila Kanisa mwanachama katika mtazamo wake na ukweli unaheshimiwa. Makanisa wanachama yamekumbatia chaguo la kutembea pamoja katika uhusiano wenye tija na uwajibikaji. Ufuatiliaji pamoja na mabadiliko ya haya maamuzi na maazimio katika makubaliano.

## Maelezo ya kikanda

- Hutoa fursa kuweka mkazo sera ya haki ya jinsia ya LWF kupitia mabadiliko ya mtazamo, mijadala na uzoefu.

Kanda hutoa jukwaa ambapo ushirika wenye tija na uwajibikaji unaweza kubuniwa kupitia mifumo iliyokubaliwa, zana na mbinu. Wanaweza kuandaa nafasi kuhakikisha kuwa mitizamo ya kienyeji inaimarishwa kwa kubadilishana uzoefu katika mtazamo.



# Kanuni ya sera ya haki ya kijinsia ya LWF

LWF ni ushirika wa Makanisa waliojitoa:

1. Kuendeleza haki ya jinsia kama msingi wa kitheologia wa kudai haki na utu kwa watu wote. Kuendeleza usawa wa kijinsia, maarufu kama haki za binadamu.

2. Kukuza thamani ya utu na haki, ujumuisho na ushiriki, uwajibikaji wenye tija na uwazi kwa kuangazia heshima kwa kuangalia na kuheshimu vipawa vya watu wote.

3. Kutekeleza katika ngazi ya kikanda na kienyeji maamuzi yafungamano na baraza la LWF. Maamuzi yanayohusiana na ujumuisho kijinsia, usawa wa vizazi kuhakikishwa usawa katika uwakilishi na ushiriki wa wanaume na wanawake katika ngazi zote za kufanya maamuzi.
4. Kuhakikisha uchambuzi wa kijinsia katika kazi zote za ubinadamu na maendeleo na kusemea kwa makusudi usawa wa kijinsia ili kuimarisha mifumo ya haki na ujumuisho. Kwa sababu hii, ni muhimu kutambua na kuchambua matokeo ya maendeleo yote na michakato katika usawa wa kijinsia.
5. Kuunga mkono uwezeshwaji wa wanawake kama mkakati wa msingi kuelekea kumaliza mgawanyo usio sawa wa mali na kuzuia ugomvi pamoja na kuzuia mizozo yenye misingi ya kijinsia.
6. Kuendeleza kwa usahihi kuhusika kwa wanaume kwa kuangazia vielelezo vya mabadiliko ili kumaliza mfumo dume na kujiuhusisha katika haki ya kijinsia.
7. Kusemea utendaji wa mifumo na miundo ambayo husababisha vikwazo vya ushiriki kikamilifu wa wanawake katika uongozi na katika ngazi za kufanya maamuzi.
8. Kuhakikisha kuwa sera ya msingi ya taasisi, mifumo, utendaji, bajeti, usimamizi wa rasilimali watu, wafanya kazi, uwakilishi, mafunzo, taasisi za uongozi na kufanya maamuzi



# Mbinu Ya Sera ya Haki ya Jinsia ya LWF

na usawa wa kijinsia na kuunga mkono ushiriki sawa wa wanawake na wanaume.

9. Kuhakikisha kuwa uchambuzi wa kijinsia umejengwa ndani ya mipango na hatua katika mzunguko wa mradi: kukagua, kupanga, utekelezaji, usimamizi na tathimini.

10. Kuhusisha vipengele vyote vya theologia, litrugia na maisha ya kujitoa katika mtizamo wa haki ya kiijinsia.

Mbinu ya sera ya haki ya jinsia ya LWF huelekeza mchakato wa kufikia haki ya jinsia.

Miongozo inayotolewa kwa muelekeo wa kufundisha hadi kuangazia haki ya jinsia zimekitwa katika mbinu katika njia tatu kuona, kutenda, na kutoa mawazo umeundwa kama utaratibu wa kutambulisha namna ya kujizatiti kwa ajili ya sera.

Maelekezo yote ya ushirika yanatiwa moyo kuchangamana katika

muelekeo wa mbinu hii, kubadilisha na kuleta katika uhalisia na lugha zao dhana hizi za msingi.

- Kuona inamaana ni kuchunguza na kusoma ukweli wote katika uhalisia.
- Kutathimini/kutambua inamaana kutumia dhana za kibibilia na kitheologia na zile zinazokubalika kwa ujumla juu ya haki za binadamu kutambua ukweli huu na masuala muhimu yanayoibuka kutoka kweye mtazamo.
- Kutenda Ina maana ni kufanya. Baada ya kusoma na kutambua ukweli wa mkakati katika mtazamo huu unakubalika

Kuona: Jumuiya inasimamia wapi katika safari ya ujumuisho sehemu hii ya kwanza hutoa nukuu za kuanzia kuhusu wapi tulipo kuhusuana na ushiriki wa wanawake na uchambuzi wa jinsia.

Inaelezea hadithi za ushiriki wa wanawake katika ushirikiano na jinsi ambavyo jinsia inakuwa zana ya kitheolojia ndani yake. Zoezi la kuangalia ukweli na kusikiliza kwa makini sauti mbalimbali katika jumuiya kuhusiana na vikwazo vya jinsia hasa ambavyo wanawake wanakabiliana nayo. Pia mwongozo ulipendekeza kama hatua ya kwanza ya utekelezaji wa sera ya haki ya jinsia ya LWF. Mchakato wa kujenga mwamko wajinsia na sera haukuanzia hewani: bali imejengwa katika "elimu" ya vipindi tofauti. Jumuiya na watu binafsi walihusika.

Kuamua/kutambua: Misingi ya kibibilia na kitheologia kwanini haki ya jinsia ni muhimu katika ushirikiano wa kilutheri? Katika ushirikiano bibilia ya urithi wa kilutheri ni vioo ambavyo jinsia inavyojadiliwa kwa mtazamo wa imani. Katika lugha ya imani, usawa wa kijinsia unatamkwa kama haki ya kijinsia. Haki ni kipengele cha kuanzia ambapo tunaweza kujadili uhusiano wa usawa. Haki ni tangazo la kinabii na ni msingi ambao unaweza kuleta mabadiliko na heshima kwa wote. Mtazamo huu wa kibibilia kuhusu haki hupenya kwenye mijadala ya kitheologia na kuangazia sehemu hii kwa ujumla. Dhana ya msingi ya kitheologia ya utambulisho wa kilutheri imechambuliwa kupitia vioo vya haki ya jinsia kutokana na mjadala huu huibua muelekeo wa kitheologia katika sera ya haki ya jinsia.

Kutenda: utekelezaji na ufuatiliaji wa kipengele hiki cha tatu huonyesha kanuni ya kimkakati na miongozo katika utekelezaji. Mpango wa kufikia haki ya jinsia kukuzwa katika vipengele saba – utangulizi wa thamani na kujizatiti ukifuatiwa na idadi ya mipango ya utekelezaji. Sera ya haki ya jinsia ya LWF imedhaniwa kama mchakato shirikishi kwa kuangazia na kufanya kazi katika haki ya kijinsia kwa kusudi la na sera hai na dhahiri ambayo inaweza ikatamadunishwa na kutumika katika kanda mbalimbali ikiwa na makinisa wanachama 142 katika kanda saba za kijiografia (Asia, Afrika, Nordic, Ulaya Mashariki na Ulaya Magharibi, Amerika ya Kaskazini, Latini Amerika na visiwa vya Karibiani), mtazamo ushirikiano una tofauti za hali ya juu. Jambo moja katika kipengele hiki ni

utajiri wa aina mbalimbali za lugha ambayo hupitiwa kwenye ushirikiano wakati kazi za kiofisi za ushirikiano zinafanyika kwa Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, na Kispaniola. Ni changamoto kuelezea katika maandishi utajiri huu mtambuka na kurekebisha hoja kwa namna ambavyo tunakuwa ni mwaliko wa kuendeleza mjadala na kujihusisha na kuwa wazi kuweka mkazo katika kweli mbalimbali. Tunawezaje kupangilia maandiko ili liweze kuibua mjadala zaidi utakaoelekea kwenye mabadiliko?

Sera ya haki ya jinsia ya LWF ni ukaribisho kujihusisha katika jumuiya za mabadiliko katika mahusiano na muundo katika Kanisa jamii na maisha. Katika ufahamu kuwa maisha huja kwanza, muongozo huu wa mbinu hutoa mipango kuhusu namna ya kuweka mkazo baadhi ya kanuni zilizofafanuliwa katika sera hii. Kwa hiyo kuanzia kuchambua ukweli ambayo mtu amekuwa nayo na kuuliza maswali na kusoma kwa namna ya kutambua mtazamo ni hatua za kwanza zinazofuatiwa na mitizamo ya kitheologia katika mjadala wa mtazamo wa haki za binadamu na vielelezo vya tathmini ya maendeleo, miundo na mila na tamaduni. Uchambuzi wenyewe hata hivyo hautoshi: kinachojalisha ni utendaji, kuleta dhana na thamani katika maisha. Kwahiyo utekelezaji na mafanikio ni matarajio na matokeo muhimu ya baadae.

Kuweka mkazo katika mila tofauti ambayo jumuiya inafanya kazi hubakia kuwa changamoto. Hata pale ambapo mila inafafanuliwa kama mfumo wa elimu mchangamano wa tabia, itikadi, thamani na ishara zilizokubaliwa na kushirikishwa na kundi la watu, inadhaniwa kuwa mtazamo huu haujadumaa bali umesambaa. Mchakato wa kutilia mkazo, hata hivyo, ni lazima itilie maanani vipengele vya kiutamaduni na mtawanyiko. Kila mtazamo utafafanua vipaumbele ambavyo vitatekelezwa katika eneo fulani: ukweli fulani hauwezi kulazimisha juu ya ukweli mwingine na kufafanua nini kitakuwa muhimu: kujifunza kwa kushirikiana kutarutubisha na kuimarisha vitendo katika maeneo yote ya Kanisa na jamii katika kufikia haki ya jinsia.

Sera hii inaleta mabadiliko gani katika maisha ya watu wanaohusika na uchanganuzi na vitendo? Ni swali la msingi linaloambatana na mchakato huu. Mwisho kusherehekea uwezekano wa kuja pamoja na kuwa na uwezo wa kujadili mabadiliko ya msingi katika maisha na theolojia ya maisha ya Kanisa. Kusherehekea umoja, kusherehekea ushirika, kuomba na kuimba pamoja,

> Mungu huwaita watu wake sasa katika maisha mapya, watembee pamoja bega kwa bega: muda muafaka wa mabadiliko umewadia, muda ni sasa. Tutembee kwa pamoja sasa hakuna anayepaswa kutembea peke yake' kwa hiyo, njoo ujiunge' (Thuma Mina 2021, Deusi

chama ejente pra um momento novo).


## Ushirikiano umesimama wapi katika safari yake ya ujumuisho?

### *Uongozi na ushiriki wa wanawake*

Zaidi ya miongo LWF imeendelea kutenda sawasawa na theologia yake na kujizatiti kivitendo kutambua ujumuisho kama moja ya thamani zake za msingi.

Hili linaonekana katika maamuzi ya awali ya kudhibitisha ushiriki wa wanawake:


## Asilimia ya Makanisa wanachama wa LWF Wanaobariki wanawake kuwa wachungaji




Makanisa yasiyosimika wanawake

Makanisa yanayosimika wanawake

## Asilimia ya wanachama kutoka Makanisa wanachama wa LWF Wanaobariki wanawake kuwa wachungaji




Wanachama kutoka Makanisa ya LWF wasiosimika wanawake

Wanachama kutoka maKanisa ya LWF wanaiosimika wanawake

*Chati iliyoko upande wa kulia huakisi idadi kubwa ya Walutheri milioni 70.5 katka jumuiya Makanisa yaliyoko chini ya LWF yanayosimika wanawake*

- Mwaka 1952 kwenye fungamano la LWF huko Hanova Ujerumani nafasi ya mwanamke ilijumuishwa na kuendelezwa kama baraza la wanawake, muanzilishi wa kamati ya ushauri wa dawati la wanawake alichaguliwa mnamo 1975. Uamuzi wa kuunda dawati la wanawake uliamuliwa 1970 katika kongamano la tano la LWF huko Ivian ufaransa. Mwaka 1984, maamuzi ya wazi kuhusu ushiriki wa wanawake na walei wa kawaida yalifanywa katika baraza la saba huko Budapest, Hungary

ambao uliamua kuanzisha "mfumo wa quota" kuhakikisha ushiriki wa angalau asilimia 40 ya wanawake. Na la 8 (Curitiba, 1990) na la tisa (Winnpeg 2003ni mabaraza yaliyo thibitisha makubaliano hayo).

- Makongamano na mabaraza, ofisi ya ushirika, taasisi za maamuzi walikubaliana kwamba karama ya wanawake katika huduma ya kusimikwa ni kitendo cha pekee ambacho kinapaswa kutimizwa katika ushirika ulimwenguni kote. Kipengele kimojawapo cha uchambuzi wa kitheologia na maana ya siku zijazo ni kwa ajili ya kuwajumuisha wanawake katika huduma ya kusimikwa. Inaonyesha jinsi Kanisa linavyojielewa lenyewe, na kuwa na ushuhuda kwa uma na kuishi kwa kutangaza injili kwa ujumla.

Ushirika wa wanawake katika huduma ya kusimikwa ni muhimi ingawa sio tu hatua ya kujenga ujumuisho katika ushirikiano. Ushiriki kikamilifu wa wanawake na wanaume katika taasisi za kufanya maamuzi ni hatua nyingine muhimu kuelekea ujumuisho. LWF hujumuisha *ecclesia sempr reformanda* utambuzi wa mchakato wa mabadiliko endelevu kwa njia mbalimbali.

Ndani ya ushirikiano juhudi nyingi chanya zilishafanyika na mabadiliko yenye msingi na maamuzi yanayounga mkono ushiriki kikamilifu wa wanawake. Kwa mfano mfumo wa Quota hukubali na kuendeleza uongozi shirikishi katika taasisi na miundo ya LWF kama vile makongamano na mabaraza. Matumizi ya quota ni utaratibu wa muundo ambao ulibuniwa kwa ajili ya kukabiliana na vikwazo vya kivitendo ambavyo wanawake wanakabiliana navyo wanapokazana kufikia hatua na nafasi mbalimbali. Kupitia uhusiano wa vikundi vya wanawake vya LWF, wanawake na wasichana wanachangia ustawi wa jamii kwa kutoa huduma za kidiakonia kwa jirani zao. Hata hivyo Kanisa bado halijaweza kushughulikia kikamilifu jinsi ambavyo mifumo na uhusiano wa kijinsia kuzalisha manufaa kwa baadhi na uonevu na maumivu kwa wengine na hivyo kuathiri maisha ya kushirikiana katika Kanisa na jamii.

Wakati mfumo wa quota ni zana nyingine ya muhimu kuhakikisha uwepo wa wanawake, vikwazo vya mara kwa mara vinabakia katika njia ya kushiriki kikamilifu. Hili linaonekana kuna mkato katika maamuzi yanayochukuliwa ulimwenguni, katika kongamano, na kile kinachoendelea kienyeji. Kutimiza quota tu haitoshi. Wakati quota inaweza ikahakikisha uwepo, si muhimu kuwa havihalalishi umuhimu wa ushiriki. Ili kuwa waaminifu kwa kongamano lililopita hujitoa na kufikia lengo la ujumuisho mkamilifu, kuna uhitaji wa haraka wa kubadilishwa wakati Makanisa na ushirikiano wa ulimwengu kwa nguvu ambayo wanawake na vijana wanachangia.

Mojawapo ya mafanikio katika maisha ya ushirikiano wa LWF ni sauti ya kinabii katika Makanisa inayosema

"*Hapana" Kwa Unyanyasaji Dhidi Ya Wanawake,* hili hudhihirisha kuwa ukatili unakuwepo katika Makanisa na kujadili hatua za kuchukuliwa kupambana na ukatili huo

Kazi ya Makanisa na taasisi za Makanisa kuhusiana na kuzuia na kushinda ukatili dhidi ya wanawake imekitwa katika maadili ya kuvumilia unyanyasaji. Vitendo vya kidiakonia na uchambuzi wa kitheolojia ni sehemu ya muelekeo – kwa imani na dini, ambayo utasaidia kuondoa hatari za mara kwa mara kati ya dini na mila ambavyo vina watenga wanawake katika maeneo binafsi ambayo ukatili kutokea mara kwa mara.
Uzoefu unaopatikana kutoka kwenye uchambuzi na utekelezaji wa mpango kazi wa LWF, Makanisa yanasema "hapana" juu ya ukatili dhidi ya wanawake,

huonyesha wazi kuwa kuna ukatili uko Makanisani. Kipengele kinachohitaji kufikiriwa katika jitihada za kuondoa ukatili. Kipengele kimojawapo cha kazi ya Kikristo ni kutaja kitu kama kilivyo. Kwa hiyo ni muhimu kuwa ushirikiano utangaze hadharani kuwa ukatili dhidi ya wanawake ni sehemu ya dhambi, na ya kwamba maKanisa yanaitwa kuwa mbingu salama.

### *Jumuiya katika njia ya haki ya jinsia*


LWF huendelea kukuza njia za kuunga mkono makubaliano yake ya kufikia haki ya kijinsia katika ngazi ya taasisi na mifumo:

- Mnamo mwaka 1997, kongamano la 9 huko Hong kong, kujitoa kwa ajili ya usawa wa kijisia kulitambuliwa kama moja wapo ya kiini cha shughuli za ushirikiano: kushughulikia jinsia na mamlaka kutoka mtazamo wa Kibibilia na Kitheologia kama suala la haki na mahusiano na kushughulikia jinsia na mamlaka kama suala la uongozi.
- Kongamano la 10 la mwaka 2003 huko Winnipeg, Canada ulikazia masuala mbalimbali yalijadiliwa na maamuzi yakachukuliwa kwa miaka iliyopita na ulikubali tena kuendelezwa wa kujumuishwa kikamilifu kwa wanawake na vijana katika maisha ya Kanisa na jamii.

---

[7]inapatikana
www.lutheranworld.org/content/resource-churches-say-%E2%80%9Cno%E2%80%9Dviolence-against-women-actionplan-

- Uzoefu wa Kanisa wa kidiakonia ulionyesha kuwa uchambuzi wa kitheologia hua dhahiri unapoambatanishwa na huruma ya ndani na kuwajali majirani. Ni kwa kupitia kazi za kidiakonia Makanisa hujiweka kwenye nafasi ya huduma kwa uma, kusikiliza, kuona, kugusa, kutambua na kuwasindikiza wale wanaoteseka na kuonewa. Katika vuguvugu hili la kutawanyika la kujihusisha na huduma_za uma na kwa kutoa tafakari ndani ya thamani ya imani tajiri maKanisa yanakuwa raia au raia wao wenyewe. Uraia wa Kanisa ni sehemu ya utambulisho



wa kitheologia, ni njia ambayo Makanisa hujielewa wenyewe kama sehemu ya vuguvugu la kudumu la Mungu juu ya uumbaji na watu wote. Ni sehemu ya kujielewa kimisheni yakutumwa ulimwenguni ambayo kwanza ulitolewa na Mungu kama hatua ya neema ya kutoka nje ya utawala wa yasiyogusika na huruma ya msingi kuingia katika furaha, mateso, maumiivu na matumaini ya ulimwengu.

- Ni kwa uelewa huu wa misheni ya udiakonia LWF hufanya kazi kuendeleza haki na usawa kamili kwa watu wote na, hatimaye, hujihusisha kuendeleza uongozi na ushiriki kikamilifu wa wanawaake. Uzoefu na mwelekeo wa kidiakonia wa kutukuza haki za masikini na walioonewa hutoa msingi wa kivitendo katika dhana ya uelewa wa haki katika ngazi zote na mahusiano yote, hasahasa kipekee katika mahusiano ya kijinsia.
- Mnamo mwaka 2009 mchakato wa uchambuzi juu ya jinsia na mamlaka ulipangiliwa na kuchapishwa kwenye waraka, “haitakuwa hivyo kati yenu ” uchaguzi wa imani kuhusu jinsia na mamlaka ambao ulipokelewa na baraza. Huu ni mfano mwingine wa uchambuzi na uchanganuzi wa jinsia na hutoa msingi ambao uendelezaji wa sera hujikita.
- Zaidi, LWF kama ushirikiano wa Makanisa, limekita maamuzi yake kuchukua sera ya haki ya kijinsia katika uzoefu na kujihusisha kwa Makanisa wanachama katika kazi zao kuelekea kuendeleza haki za binadamu. Makanisa na taasisi za Kikanisa sera ya kijinsia ni msingi wa kukuza sera pana ya jumuiya – ni vuguvugu ya mzunguko. Uzoefu unakusanywa na kupangiliwa katika ngazi ya ushirikiano. Kuanzishwa kwa makubaliano ya jumuiya imekitwa katika makubaliano na uzoefu huo.

Somo mipango hii na michakato yote huwepo katika ngazi zote za ushirikiano – Makanisa wanachama, maofisi, mipango na miradi- ni changamoto katika kuangazia muelekeo kwnye ufahamu zaidi, uliokitwa katika dhana za kitheologia, kwa namna ya kushughulikia njia ambazo mifumo hii ya manufaa na uonevu uliokitwa na kujengwa juu ya mifumo jamii na mila, huathiri uwepo wa wanawake katika uongozi inakwenda mbele zaidi ya kuvuka ufahamu wa “kuwaleta wanawake mezani” (uwepo) kuelekea “usawa wa hali wa wanaume na wanawake mezani” (ushiriki kikamilifu).

## Misingi ya Kibibilia Na Kitheolojia: Kwanini Haki ya Kijinsia Ni Muhimu Katika Ushirikiano ya Kilutheri?

Kukuza na kuchukua sera ya haki ya kijinsia katika jumuiya ya LWF ni sehemu ya mchakato wa kuelewa misheni kamilifu kama mfano wa neema ya Mungu ulimwenguni. Theologia ya kilutheri ni tajiri katika rasilimali kuimarisha uelewa wa ushirikiano kuhusu uwajibikaji wa

pamoja juu ya haki ya kijinsia kama tendo la imani.

Utamaduni ni sehemu ya sifa kuu ya theologia ya kilutheri, ndani ya LWF, Hii ni kumaanisha mijadala inayoendelea kikanda. Kwa mujibu wa mkakati wa LWF wa 2012 hadi 2017.

> Mahusiano ya jumuiya yanategemeana kuna vituo mbalimbali vya maamuzi na mipango. Kila sehemu ya jumuiya husaidia kuwawezesha Makanisa wanachama kushiriki na kujenga maisha ya jumuia kupitia mtandao unaowaunganisha na kuwaleta pamoja kikanda na kiulimwengu. Tofauti zao tajiri za kiutamaduni unapaswa kusherehekewa na kutoa fursa za aina mbalimbali kushirikiana na kuchangamana, changamoto za pamoja, na kujifunza kwa pamoja[8]

Haki ya kijinsia ni hatua ya kuanzia kati ya vituo hivi vingi na mijadala kati yao.

Sura ya kibibilia ya usawa na haki uliwasilishwa mwanzoni mwa sera hii (uk. 5) kama msingi wa kibibilia wa uelewa wa ushirikiano wa LWF kuhusu jinsia na haki. Wanadamu waliumbwa kwa sura ya Mungu. Mume na mke: tofauti bali wako sawa. Wanaume na wanawake wanashiriki manufaa na wanawajibika kutunza uumbaji wote wa Mungu. Wanadamu humtegemea Mungu na kwa hivyo watumikiane kila mmoja kwa mwenzake.

---


[8] Op. cit. (note 4), 9.

Kutumia zana ya jinsia kufafanua hadithi ya uumbaji inaweza kuibua maswali ya tafakari kama vile: wanaume na wanawake wanakubalije utu Kwa Mungu katika uhusiano wa wanadamu wote? Wanaume na wanawake waishije na kuwa washirika na Mungu katika kazi endelevu ya uumbaji? Kiini cha dhana za kibibilia cha uumbaji sawa na uwakili sawa unafafanuliwaje ili kuendeleza ushirika? Uwakili wa neema ya Munguu una maana gani katika mazingira ya utamaduni wako? Ni nini mtazamo wa uwakili wa haki za wanawake na wanaume katika mazingira ya utamaduni wako?

Ifuatayo ni baadhi ya misingi ya kitheologia ya Kilutheri kama vipengele vya kuanzia Makanisa wanachama wa LWF wanahimizwa kukuza na kushiriki na kila mmoja wao kuhusika kwao kulikotawanyika na haki ya jinsia. Michakato na mijadala hii itatokea vizuri katika ushirikiano mkamilifu kati ya wanaume na wanawake.

### *Maandiko matakatifu: mjadala kati ya maisha na andiko.*

Kwanini Bibilia ni ya muhimu? Bibilia huzungumzia habari ya neema ya Mungu kwa ulimwengu. Luther



muhimu ni ahadi za Mungu na neema kupitia Kristo Yesu. Katika utamaduni wa kilutheri swali la msingi ni, nini kinachombeba Kristo? Kwa maneno mengine neema ya Mungu inadhihirishwaje? Hili limefafanuliwa katika injili. Yesu alipomponya mwanamke kilema hadhi yake ilihuishwa kikamilifu (Luka 13: 10-17).

Mawazo haya huibua maswali kama vile, Ahadi ya neema ya Mungu inamaanisha nini kwa wanaume na wanawake? Neema ya Mungu hutaarifuje usomaji na ufafanuzi wa maandiko ya kibibilia kutoka kwenye mtazamo wa haki ya jinsia?

Sanaa ya kufafanua ujumbe tofauti wa Kibiblia kwa kuchangamanisha na mtazamo wa siku za leo unaitwa fafanuzi (hermeneutics).

aliwakumbusha wakristo kuwa kilicho

> Utamaduni wa kiluteri unaalikwa na mtazamo wake mzuri wa kuwa na mtawanyiko kujikosoa yenyewe na kufungua wakati ujao. Mtazamo wake wa nje wa kitheolojia unaashiria kwa utambuzi wa mivutano, ambayo kuvumilia maazimio kwa sababu huangazia maeneo tofauti ya maisha pamoja na Mungu na ulimwengu wa Mungu. [9]

Kuna sehemu tofauti ya mafundisho ambayo walutheri wataona ni ya msaada katika kufafanua maandiko matakatifu. Kwamba wakristo ni makuhani, kuokolewa kwa neema kwa njia ya imani, tofauti kati ya sheria na injili *solus kristus*, *sola gratia, sola fide verbo* na Theolojia ya msalaba na kanuni ya ufafanuzi kwamba andiko hufafanua andiko. Kama ilivyobainika hapo juu, kipengele cha muhimu cha kuingilia, na ufunguo wa ufafanuzi, ni kusoma andiko kwa kuangaziwa na swali hili,

---

[9] Ibid., 8.

Je, Ni nini kilichombeba Kristo?

Kusoma biblia kwa binafsi au katika vikundi, makanisa na jumuiya huhitaji ushirikishwaji hai pamoja na andiko – vyote viwili mtazamo wa kihistoria na ule wa ukweli wa maisha halisi ya leo. Mtawanyiko na utajiri huu wa uzoefu wa maisha umeunganishwa katika mazingira ya jumuiya kati ya maisha na bibilia. Kwa hiyo, lugha na mtawanyiko wa kitamaduni katika ufafanuzi wa maandishi na wa mazungumzo pamoja na mapokeo ya msikilizaji ni vipengele vinavyohitaji kufikiriwa katika kutafsiri maandiko. Ufafanuzi wa andiko la Biblia katika mazingira ya ushirikiano ni pamoja na vitendo vilivyopo na hali ya kimazingira vitapaliliwa.

Katika jumuiya ya kilutheri kuna njia tofauti za kufafanua bibilia. Baadhi yao ni kusoma kimuktadha au kusoma kwa hali maarufu ambapo jumuiya na mtazamo ni vipengele vya kuanzia kwa ajili ya mjadala na andiko kwa kusaidia kugundua mvutano kati ya sheria na injili. Zana za kukosoa ni vipengele vya thamani kwa nia ya kuibua mabadiliko katika mifumo ya uonevu. Njia hii ya kusoma biblia inaweza ikawa ni nuru na nguvu kwa kuwawezesha wanawake na makundi yaliyotengwa na kuendeleza haki ya kijinsia. Kusoma maandiko ya kibibilia katika mtazamo wa kiutamaduni na watu vikundi vilivyo tengwa ni zoezi la kuwezesha linalokazia zaidi theolojia.

Watu wataanza kuona matatizo yao ya kila siku yakiunganishwa na hadithi za kibiblia kuhusu kuchangamana na hadithi za kibiblia. Kuchangamana na andiko inakuwa ni motisha ya kuhoji unyanyasaji unaoelekea katika jinsia. Suala la haki ya kijinsia lina misingi ya kitheolojia katika ushuhuda wa kibiblia na tamaduni ya kikristo wakati utamaduni huu wa kitheolojia na ki biblia inaweza ikafafanuliwa kama ni ya kukubali ushirikiano kati

ya wanawake na wanaume katika maeneo mbalimbali ya uongozi duniani. Hitimisho hili kwa ujumla halitendewi kazi katika mtazamo wa kifamilia, Kanisa na eneo la uma. Wanawake wanalemewa na majukumu ya kinyumbani. Wanatengwa kutokana na uongozi katika huduma na hawatiwi moyo kushika nafasi za uongozi katika eneo la uma.

Katika eneo la uma baadhi ya maandiko ya kibiblia na tamaduni za Kanisa – kutengwa huko kwa wanawake kunaweza kuhitaji kusomwa tena kwa nuru ya uelewa wa ujumla wa usawa wa wanadamu wote mbele za Mungu. Mamlaka ya Mungu kwa wanadamu kuhusu uwakili na utambulisho mpya kupitia ubatizo.

Changamoto zinazohusiana na utafsiri na ufafanuzi wa kiutamaduni ambao hauzoelewi tu katika jamii ya kisasa lakini pia ni dhahiri katika maandiko ya biblia na tamaduni za wakristo wa awali wenyewe kusoma andiko la Bibilia kwa mtazamo kwa kutumia uchambuzi wa kijinsia ni mbinu yenye msaada kwa kufanya tofauti dhahiri kati ya wanawake na wanaume katika jamii na Kanisa la leo. Usomaji wa hoja hufanikisha uundaji kwa upya wa dhana kwa dhana ambayo huendeleza mfumo wenye kuwanufaisha ili kuwanufaisha baadhi na kuwaonea wengine, kama ilivyo katika miundo ya mifumo duni. Kusoma kwa hoja kunalengo la kuwahamasisha wanawake kuelekea kwenye uhusiano wa mabadiliko wa dhana ya haki wavulana na wanaume, wasichana na wanawake katika ushirikiano. Uhusiano huu wa kijumuiya unaweza ukawa ni mfano dhahiri kwa kufafanua utekelezaji wa haki na hadhi.

- Maandiko husema nini kuhusu haki?
- Ni andiko lipi la Kibiblia linalounga mkono haki ya jinsia?
- Ni andiko lipi ambalo ni kinyume au changamoto kulinganana na uhusiano wa haki na usawa kati ya wanawake na wanaume?
- Neema ya Mungu inaweza kuwa na maana gani unaposoma maandiko haya yote?

### *Kuhesabiwa haki na neema: Uhuru na heshima kwa watu wote*

- Kuhesabiwa haki kuna maana gani?
- Kuna maana gani ya kuwa mtu binafsi aliye hesabiwa haki wakati huo huo ni mwenye hatia?
- Je matokeo ya watu binafsi na Kanisa lenyewe ya kuhesabiwa haki na kuwa na hatia ni nini?

Mwelekeo wa kitheolojia uliopendekezwa katika sera hii hutegemea haki kama dhana ya msingi – katika theolojia ya kibibilia mtazamo wa kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya imani, ambayo ni msingi wa utambulisho wa Kilutheri kuhesabiwa haki ni kuwekwa huru kutokana na kile kinachotufunga ( Rum 5).

Mtazamo huu wa theologia uliokitwa katika kuhesabiwa haki pia

hutambua kuwa wanadamu bado wanatawaliwa na mifumo na miundo isiyo haki hadi kufikia kipengele cha kushikiliwa na sheria isiyo haki: hatimaye kuishi katika dhana ya msingi ya kuhesabiwa haki kwa neema ya Mungu ni kuwa huru kutoka utawala wa kisomi au kukamilisha matakwa ya utamaduni wa mfumo dume. Hivyo tunahesabiwa haki na kuwa na hatia hapohapo – *simuliustus ete peccator.* Kutokana na mtazamo wa Kilutheri hii ni hali tata ambayo Kanisa na jamii hujikuta wakiwemo. Kuongozwa na msukumo wa neema ni kuthibitisha kuwa wanawake na wanaume wanawezeshwa kuvumilia na kujihusisha kwenye vitendo vya mabadiliko.

Wanadamu sio tu kwamba wako sawa katika uumbaji, lakini pia katika dhambi. Paulo anafafanua, "kama ilivyoandikwa: hakuna mwenye haki hata mmoja, kwa maana wote walitenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Rum 3:10, 23). Ingawa ni kawaida kuelewa dhambi kwa mtazamo wa vitendo vya mtu binafsi lakini jamii na taasisi zimesahau hili.

Dhambi ni madhara tunayowafanyia wenzetu, kwetu binafsi na kwa Mungu. Sheria, tabia, mawazo, mwenendo pamoja na sera vinaweza kuwa dhambi kama vitaathiri sehemu yeyote ya uumbaji wa Mungu. Kwa hiyo dhambi sio tu jambo la mtu binafsi bali pia ni la kimuundo na kitaasisi. Jambo lolote linaloweka thamani ya kundi moja la watu juu ya wengine ni dhambi kwa sababu kuwadhalilisha wengine kuna madhara. Katika hali hii, mfumo unaokitwa kwenye utawala na uonevu, kuweka thamani ya mwanaume juu ya mwanamke, ni mfumo wa dhambi. Uelewa huu wa mfumo wa dhambi ni kama kwa uonevu kunasaidia kuepuka kutorahisisha zaidi uchambuzi. Kuishi katika mfumo kuna maanisha kushinda muundo usio haki ni jukumu la wote wanaume na wanawake. Kwakuwa mfumo wa dhambi unawadhalilisha wanaume na wanawake ni shughuli ya pamoja kushiriki katika vuguvugu la mabadiliko na matengenezo. Haki ya jinsia hata hivyo hujerea wote wanaume na wanawake, wote wakipanga maisha kwenye msingi wa ushirikiano na haki.


Kuhesabiwa haki kwa kupitia neema ya Mungu kunabadilisha maisha ya mkirsto katika dunia na kwa hiyo hulipa Kanisa msingi wa kushughulikia mifumo isiyo haki. Katika hadithi ya watenda kazi katika shamba (Mat 2:1-16), neema ya Mungu iliwaangukia wafanyakazi wote kwa sababu utu ulizingatiwa. Hivyo wanadamu wako sawa katika ukombozi.

- Unadhani kuna mabadiliko gani yaliyotokea katika maisha ya wafanya kazi kwa sababu walihudumiwa kwa usawa?
- Ni mabadiliko gani katika ushirikiano kwa sababu wote wamehesabiwa haki kwa neema ya Mungu?

### *Kufanyika mwili kwa Mungu: haki na kielelezo chake*

- Unaona uhusiano gani kati ya umoja wa Mungu na Kristo katika haki?
- Unaona uhusiano gani kati ya – wanadamu na haki?

Mungu alitamani kushiriki maisha ya mwanadamu kikamilifu katika mwili wa mwanadamu. Mungu anakutana na wanadamu katika Yesu Kristo, ambaye humwonyesha Mungu ni nani: Mungu anayetaka kuwafungua watu kutoka utumwani, kuwafungua katika vifungo vya dunia iliyoanguka, kuwawezesha masikini na walioonewa na kuwakaribisha wote kuwa na maisha ya uhuru kama watoto wa



Mungu. Huu ni uzoefu wa Mungu: kusikiliza na kushuka chini kuwakomboa watu wanaolia kuomba msaada (Kut 2:24:3:7). Yesu Kristo aliwaita wanafunzi wake katika kielelezo kipya cha familia ya Mungu, ambayo uongozi wa kibayolojia katika mfumo wa kifamilia ulibadilishwa (Mk 3:35). Mwili wa mwanadamu kwa ukweli wake wote, mateso na furaha ni katikati ya ufunuo wa kikristo kwa sababu ya Mungu kufanyika mwili kwa njia ya Yesu Kristo. Hivyo, kupitia kufanyika mwili kwa Mungu kuanzisha uhusiano wa kina na wanadamu wote. Neno takatifu huchukua mwili wa mwanadamu na kukaa ndani mwetu (Yn 1:1-14). Kuwezeshwa na Roho Mtakatifu mwili wa Kristo ni mpya jumuiya ya haki ya dada na kaka. Jumuiya hii, Kanisa, ni mwili wa Kristo leo (1kor 12:26-27). Roho Mtakatifu huwezesha Kanisa kufanya haki ionekane ulimwenguni. Haki – ni utambulisho wa Kanisa. Katika maisha ya Kanisa, wanadamu hupata - picha ya jinsi Kanisa na uumbaji wote unavyopaswa kuwa. Ni jukumu la kinabii la Kanisa kutambua muundo ambao haki inapaswa kuonekana kati ya wale wote wanaoteseka kwa ajili ya ubaguzi na ukatili. Hili husukuma na kutia nguvu Kanisa kushiriki kikamilifu katika haki kwenye mahusiano yote.

Katika mazingira yako unaona taswira zipi za Mungu kufanyika mwili?

- Taswira za Mungu kufanyika mwili zinahusianaje na haki kati ya wanaume na wanawake? (au ni kwa njia zipi kufanyika mwili kwa Mungu kunahusiana na haki kati ya mwanaume na mwanamke?).

*Sakramenti: kuwa huru kuhudumu katika meza ya mduara yenye ujumuisho.*

- Mungu anaahidi uhuru wa aina gani katika sakramenti? Katika kushiriki sakramenti takatifu unaona picha zipi za utofauti katika mwili wa Kristo?

Kupitia ubatizo kila mtu anakuwa sehemu ya mwili wa Kristo (1kor 12). Kila mtu ni muhimu na amepewa kipawa na Roho Mtakatifu kwa vipawa tofauti, uwezo, ufahamu na ujuzi.

Yesu alishiriki mezani pamoja na waliotengwa, walioonewa na wenye mahitaji alipovunja mkate na aliwawezesha kupitia mkate na mvinyo. Tunashiriki meza hiyo hiyo na kutambua kuwa tuko sawa na yakuwa ushirikiano wetu hutegemea neema ya Mungu tu. Katika Yesu Kristo wote wanapokea msamaha na maisha mapya. Kwahiyo hakuna sababu ya kuhalalisha muundo wowote wa kuwa bora, ubaguzi au uonevu kati ya wanawake na wanaume au kati ya watu na mazingira. Kama Paulo alivyofundisha kwa umaarufu wa Kanisa la Galatia na Korintho "…hamna tena mtu mume au mtu mke" (Gal 326-28: 1kor12:13).

Wanadamu wote pasipo kujalisha jinsia maumbile au hali, Wanabadilishwa na neema ya Kristo, msamaha na maisha mapya. Tofauti ya mamlaka yenye misingi ya ukabila,

daraja na jinsia yanabadilishwa – kupitia ubatizo. Wote ni mmoja katika Kristo. Zaidi Paulo anawakumbusha wagalatia “kwa uhuru Kristo alituweka huru” (Gal 5:1). Ukuhani wa waaminio unamaanisha kuwa watu hawakuwekwa huru tu bali pia waliiitwa na Roho Mtakatifu. Kutunza uhuru na utawala wa Mungu. Uhuru ni kutumika, kuunda na kuishi katika jumuiya yenye usawa kutunzana sisi wenyewe, kushirikiana vipawa na maamuzi na kuwawezesha wale waliotengwa na mifumo ya maslahi na uonevu. Haki ya jinsia ni udhihirisho wa uhuru wa kiKristo. Kwa mujibu wa Kanisa linavyooneka kuna jukumu la kushirikiana kati ya wanawake na wanaume. Kukuza miundo ya ushirikishwaji uwazi na uwajibikaji ambavyo ni vipengele vya msingi katika maisha ya watu na taasisi.

- Je ubatizo na ushirika mtakatifu unatabirije na kufungua njia mpya ya maisha?
- Ni vitengo gani vya uongozi wa kushirikiana vinaweza vikaendelezwa katika mazingira yako?

### *Nguzo za Kikanisa: kushirikiana uongozi na uanafunzi ulio sawa*

- Unafikiri ni kwa njia zipi ubatizo unaweza ukaathiri uongozi na uanafunzi?
- Sisi kama Kanisa tunaitikiaje mistari yenye kukinzana kuhusu uongozi wa wanawake?

Kupitia ubatizo wanaume na wanawake wanarejeshwa kwa Mungu. Wote wanakubaliwa na Mungu ingawa ni watenda dhambi kwa wakati huohuo. Kwa maneno mengine, kuna umoja wa kijinsia mbele za Mungu, katika hali yetu ya dhambi na utakaso pia. Kila mmoja

Ana manufaa ya kijinsia mbele za Mungu. Hakuna anayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa ajili ya kile alichokifanya au kwa jinsi alivyo, bali ni kwa neema ya Mungu tu.

Hii sura ya kushirikiana na ubunifu inadhaniwa katika sehemu yote ya mwanadamu hata kama kuna tofauti

Ana manufaa ya kijinsia mbele za Mungu. Hakuna anayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa ajili ya kile alichokifanya au kwa jinsi alivyo, bali ni kwa neema ya Mungu tu.

Hii sura ya kushirikiana na ubunifu inadhaniwa katika sehemu yote ya mwanadamu hata kama kuna tofauti ya majukumu au wajibu ambao umetengenezwa na athari za kiutamaduni. Kuwatumikisha jinsia dhidi ya nyingine hauendani kikamilifu na roho ya uumbaji. Hata kama wengine wamechukulia kurejelea "msaidizi wa kufanana naye" (Mwanzo 2:18) haimaanishi utii wa wanawake kwa wanaume, inaweza pia ikamaanisha uaminifu katika kusaidiana kwa sababu katika maandiko mengine neno hilo hilo "msaidizi" linatumika kumaaisha Mungu. Kwa mfano, "nitayainua macho yangu kutazama milima. Msaada wangu utatoka wapi *(ezer)?* Msaada wangu (*ezer)* unatoka katika Bwana aliyezifanya mbingu na nchi" (Zaburi 121:1-2). Hapa neno lilitumika kwa mwanamke kama msaidizi wa mwanaume limetumika pia kwa hali ya kumtegemea Mungu. Katika zaburi 121. Kulingana na huu uelewa, msaidizi hafahamiki kwa namna ya mtii bali kutegemeana katika kusaidiana.

Na maelekezo kwamba "wanawake wanyamaze Kanisani" (1 Kor 14:28)[10]. Pia kuhusu manabii, mtu mmoja tu ndiye anayeruhusiwa kuzungumza kwa wakati mmoja na kama mtu ana ufunuo wakati mwenzake anaendelea kuongea "mtu wa kwanza anyamaze kimya" (1kor 14:30). Kwa hiyo, katika Wakorintho kuwanyamazisha wanawake inaweza ikatazamwa kwa mtazamo mpana kama kupangilia ibada hata kama "sheria"



[10] Baadhi ya tafiti husema ukweli kwamba maandiko haya hayawezi kuhusishwa na Paulo, lakini ni

nyongeza katika kitabu, ni kuingizwa kwa kujenga baadaye hoja ya kutengwa na ukimya kwa ajili ya wanawake. Angalia, kwa mfano, baadhi ya machapisho ya Elizabeth Schüssler Fiorenza.

au mpangilio wa uumbaji zimetumika kama njia ya kukazia hitaji hili.

Maelekezo ya Paulo kwamba wanawake wanyamaze katika mikutano Makanisani imesukumwa na mtazamo haiwezi kueleweka kama sheria ya ujumbe kwa kuwa Paulo anaunga mkono wanawake kuzungumza katika mikutano ya umma (1kor 11:5). Kuna mkinzano wa wazi maandiko hayo mawili ambayo kwa uwazi inaonyesha kuwa katika vipindi vya biblia kama ilivyo sasa, mtazamo hubaki kuwa kipengele muhimu katika ufafanuzi.

Kwa uwazi, kulingana na mtazamo wa kihistoria ambayo iliandikiwa, mazingira ya maandiko ya agano jipya hayaungi mkono usawa wa kijinsia maandiko yanayopuuzia muundo wa kijinsia (kwa mfano matakwa ya wanawake kunyenyekea kwa waume zao katika (Efeso 5:21-24:kol 3:18) yanapaswa kuchunguzwa kwa undani kwa kuangazia mafundisho katika utamaduni wa maneno au misemo ya kikristo na nyaraka za Paulo.

Acha tuthibitishe kuwa ubaguzi wowote wa uongozi wa kijinsia hauendani na biblia na utamaduni wa Kanisa? Kuna wanawake ambao walikuwa ni watumishi wa Mungu katika agano la mwanzo katika vipindi vyote vya maagano yote mawili, Agano Jipya na Agano la Kale. Kulikuwa na “Miriam nabii wa kike” (Kutoka 15:20) ambaye alifanya kazi na Haruni na Musa. Kulikuwa pia na Debora, ambaye alikuwa kiongozi wa kidini na wa kisiasa pia (Waamuzi 4:4). Nabii wa kike Ana alithibitisha umasihi wa Yesu na alimbariki alipokuwa anawekwa wakfu Hekaluni (Luka 2:36). Yesu alikuwa na wafuasi wengi wanawake na wanaume. Wafuasi wengi wa kike walihusika na mahitaji ya Yesu ya kiuchumi:

> Maria aliyeitwa Magdalena ambae alitokwa na pepo saba na Yoanna mke wa chuza msimamizi wa nyumba ya Herode na Suzana na wengine wengi ambao waliwasaidia kwa namna mbalimbali (Luka 8:2-3 pia Marko 15:41).

Wengi wa wanawake hawa walikuwa ni mashadi wa kwanza wa ufufuo(Luka 24:22: Yohana 20:11-18). Katika Warumi 16 wanawake wengi walitajwa katika kazi na huduma mbalimbali pamoja na ile ya kuwa watumishi wa Paulo kama vile Priska (warumi 16:3), na mitume Junia (Warumi 16:7). Wanawake walishika nafasi za uongozi katika jumuiya za kikristo kwenye karne ya kwanza. Katika historia ya Kanisa, wanawake wengi walipitia mateso kwa sababu ya ushuhuda wao kwa Kristo (kwa mfano, Papetua na Felista).

Kanisa kama kioo cha utambulisho wa kijamii, hutoa mwongozo wa ufafanuzi wa utamaduni kuhusu nini maana ya kuwa “uwanaume” au “uwanawake”. Kunyamaza na kutokuchukua hatua kwa Kanisa ni

vitendo vya kubweteka. Katika kiini



cha moyo wake Kanisa halikutumia rasilimali za kitheologia ambazo hukuza utu na kushamiri kwa wanadamu na zenye matokeo ya kubadilishwa kwa vitendo vinavyowabagua wanawake na baadhi ya wanaume katika msingi wa itikadi za kijamii na kiutamaduni.

- Ni kwa njia zipi sisi kama Kanisa tunaruhusu mafafanuzi yasiyoendana na Biblia kuathiri na kuendekeza itikadi hasi za kijamii na za kiutamaduni katika Kanisa na jamii?
- Kwa msingi wa hadithi za kibiblia ni kwa namna gani na ni wapi tunaweza tukatekeleza haki ya kijinsia katika mtazamo wa Kanisa?

## Miongozo na zana za kujikita katika mpango kazi

Kusimamia na kuwajibika: Ofisi Ya Ushirikiano itakuwa inawajibika kwa ufuatiliaji wa kitaasisi na usimamizi kuhusu kazi za programu. Mapitio ya maendeleo yatapaswa kuwasilishwa kwenye baraza na katibu mkuu.

Kipengele hiki cha sera ya haki ya jinsia cha LWF hutoa zana za kivitendo na mwongozo wa kuchambua jinsia kwa Jumuiya zote za Kilutheri. Baadhi ya zana za kivitendo zinapendekezwa badala ya kuelekezwa. Zana za kivitendo na mwongozo vinaweza kutumika kuendeleza ushirikiano wa majukumu na wajibu katika ngazi zote na kati ya viongozi na vikundi katika makanisa wanachama na pia kwa wafanya kazi wa ofisi jumuiya na ofisi ya

huduma za dunia na katika programmu ya nchi.

Ili kufikia lengo la haki ya kijinsia katika ngazi zote – kama ilivyo kubaliwa katika mkakati wa LWF wa 2012 – 2017. LWF imejizatiti kwa ajili ya thamani ya utu na haki kwa wote, huruma na kuheshimu utofauti, ujumuisho na ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji ambao unaimarisha kazi zake na dhamira yake.

Hapa chini kumeorodheshwa mikakati ya utekelezaji wa haki ya jinsia.

*Tathimini ya mtazamo*

Kutambua mtazamo tofauti ni hatua ya kwanza ya kuchukua katika kuingilia kati kitheologia, kiubinadamu au kimaendeleo. Ili kuiendeleza sera yeyote kama sehemu ya mpango kazi wa taasisi, cha kuongoza kazi za programmu, muelekeo wa mbinu unapaswa ukitwe katika kusikiliza kwa makini uzoefu wa maisha ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana, na uchumi wa jamiii, muktadha wa kisiasa na kiutamaduni ambayo unawaathiri wao. Katika mchakato huu wa tathimini wa mtazamo, ni muhimu kutambua kuwa, miongoni mwa unyanyasaji wa kijinsia katika ulimwengu mara nyingi umeelekezwa dhidi ya wanawake. Kwa hiyo, mkazo unapaswa kuwawezesha wanawake pamoja na kushirikisha wanaume ili kufikia haki. Uzoefu unajengwa kiutamaduni na mara nyingi huashiria kutowiana katika uhusiano wa mamlaka. kutaja na kuchunguza mamlaka haya kwa kuhusianisha na uchambuzi wa kijinsia hutoa taarifa kuamua ufanisi wa mikakati katika tathimini ya mtazamo.

uchambuzi wa jinsia unafafanuliwa kama:

- Zana ya kuelewa tofauti kati ya ukweli kati ya wanawake na wanaume.
- Uchunguzi wa tofauti unaopelekea ubaguzi na kutowiana kijamii, kiuchumi na kisiasa na kidini.
- Ni zana inayotambua mgawanyo wa kazi unaoangalia jinsia na maelezo ya wanaume na wanawake, kwa kufikiria tofauti zao katika hadhi ya kijamii, mahitaji ya kibaolojia, kiuchumi katika hali na ukabila na /au utambilisho wa kijinsia nk. Kama sehemu ya mchakato wa kufikia usawa wa kijinsia. Matokeo yaliyokusudiwa ya uchambuzi wa jinsia ni kubadilisha mamlaka yasiyowiana kimahusiano kuwa

katika uhusiano wa haki kati ya wanawake/ wasichana na wanaume/ wavulana.

Kwa hiyo kuna hitaji la:

1. Kukusanya na kuchambua takwimu ambazo zina ubaguzi wa kijinsia ili kutambua kutokuwiana kijinsia katika maeneo yote ya binafsi na ya uma.
2. Kukita ubunifu wa suluhisho la miradi na programmu katika matokeo ya uchambuzi wa takwimu.
3. Kutumia zana za uchambuzi wa kijinsia na tathmini ya madhara ili kugundua mifumo iliyoelekea kijinsia ya kufikia na kumiliki rasilimali na manufaa yataarifu sera na maamuzi ya utawala ambayo yataondoa kutowiana na kukuza vitendo vya usawa.

### *Mkabala shirikishi*

Uonevu wa kijinsia unahitaji kushughulikiwa kwa haraka sana. Mijadala inayohusisha na inayoshughulikia uchunguzi katika masuala ya kijinsia na inayokuza mabadiliko inayopelekea utendaji wa haki ya kijinsia huchangamotisha itikadi za mfumo dume na ambazo hajumuishi katika Kanisa na jamii vinapaswa kutiwa moyo.

Kuanzisha ushirikiano mpya na kuimarisha uliopo ni muhimu kwa ajili ya mjadala ili mabadiliko yatokee. Haya mazungumzo ni muhimu ndani ya na kati ya jumuiya, familia, makanisa wanachama, na vituo vyote vya LWF na kati ya maelezo ya LWF na taasisi za jumuiya ya Makanisa ili kushughulikia usawa wa kijinsia kama hitaji la msingi kwa ajili ya dhamira kamilifu.

Katika ngazi ya utendaji, ushirikishwaji unahakikishwa kupitia programmu na miradi na kazi za Makanisa wanachama:

1. Kutoa nafasi na jukwaa kuwaleta wanaume na wanawake pamoja na /au kuwatofautisha na kuwasikiliza kwa undani, kuchunguza kwa makini na kuelewana kila mmoja wao kuhusu jinsi watakavyochukulia na kutabiri ukweli wao na kile ambacho kila mmoja anakipitia.
2. Kuzoeza kazi kujenga vikundi na ushirika kati ya wanaume na wanawake, kwa kujumuisha zana na mbinu za utatuzi wa matatizo.
3. Kuhakikisha kuwa haja za kimkakati na mahitaji ya kivitendo ya wanawake na wanaume, wavulana na wasichana zimeshughulikiwa kwa usawa katika mzunguko wa mpango wa mradi: na wote wanaume na wanawake wanaonekana katika majukumu yao ya uzalishaji na uzaaji.

### *Haki ya jinsia ya mkato*

Kutangaza haki ya jinsia kama mkato wa kipaumbele ni mkakati wa msingi wa kisiasa na wa kimaamuzi[11] inamaanisha kwamba kila mchakato,

muundo, mpango, program na mradi unapaswa kuwajibika kwa haki ya jinsia vilevile na mtiririko katika kupanga kutekeleza, kusimami, kutoa taarifa na kutathimini kwa ujumla wa taasisi. Inamaanisha pia mabadiliko ya makusudi ambapo uchambuzi wa kijinsia ni kipengele muhimu katika mchakato wa kufanya maamuzi ufafanuzi rasmi wa UN kuhusu uchambuzi wa kijinsia ni ufafanuzi uliojumuishwa katika ENCOSOC hitimisho iliyokubaliwa 1997 ambapo uchambuzi wa jinsia

[11] Cf. *LWF Strategy*, op. cit. (note 9).

umeelezewa kama "mchakato wa kutathmini hali ya kawaida kwa wanawake na wanaume. Mkakati wowote uliopangwa ili kwamba wanawake na wanaume wanufaike kwa usawa na kutokuwiana hakuendelezwi".

Ifuatayo ni hatua ya kujumuisha haki ya jinsia katika ushirikiano:

1. Michoro na bidhaa za program na mradi na mapitio ya sheria na vyombo vingine vya kisheria, nyaraka, sera za rasilimali watu, sera za lugha, na kadhalika hutumia haki ya jinsia kama zana ya uchambuzi.
2. Fafanua viashiria makini vya jinsia (kiasi na thamani) kupima manufaa na athari za program na misukumo ya wanaume na wavulana na wanawake na wasichana.
3. Kufafanua watu au kikundi walengwa katika taasisi wawe wanawajibika kusimamia mchakato.
4. Kuendeleza ufafanuzi wa kitheologia kuhusu haki ya kijinsia.

### *Kuendeleza Uwezo*

Ni muhimu kuwa wanawake na wanaume wawe na fursa sawa kikamilifu kushiriki katika uongozi na kufanya maamuzi kwa usawa. Kuwathamini wanawake na wanaume kunamaanisha kuwa Kanisa linafanya kazi kuelekea kushirikiana wajibu na majukumu na kuwawakilisha na kuwajumuisha wanawake na wanaume hadhi yao katika Kanisa na jamii. Katika maadili yake na utendaji Kanisa linaweza na ni lazima kutenda na kuweka mfano, hivyo huonyesha kwamba mipango yake inaendana na mahubiri yake ya kinabii.

Hili huwezesha Kujitoa kwa taasisi kujenga na kuimarisha uwezo kwa wanawake na wanaume kuwatia nguvu na kuwawezesha kufikia malengo ya utekelezaji wa haki ya kijinsia. Ngazi tofauti za kuendeleza uwezo zinapaswa kufikiriwa, na kwa kuzingatia mtawanyiko na mchangamano wa ushirikiano. Mikakati ya kujenga uwezo kwa mtazamo wa haki ya jinsia:

1. Kuibua ufahamu au uelewa kuhusu ukatili dhidi ya wanawake, ukatili wa majumbani na ukatili wa kijinsia.
2. Kuwakazia wanaume na kuwaangazia vielelezo vya

wanaume kuibua ufahamu juu ya masuala ya kijinsia na haki sawa na hivyo, katika ngazi ya taasisi kuwa tazama wanawake na wanaume kama viumbe walioko hatarini.

3. Kuunga mkono mijaladala ya vikundi vya masomo ya biblia kuhusu masuala ya kijinsia yanayokitwa katika maandiko matakatifu.
4. Kufungamanisha haki ya jinsia katika mtaala na programmu ya mafunzo katika seminari na taasisi za kitheologia.
5. Kuendeleza mafunzo katika ngazi rasmi na isiyo rasmi kwa ajili ya walimu, wanaojitolea, watumishi wa masuala ya kibinadamu, wachungaji na watumishi wa Kanisa, kuwawezesha wawe makini katika masuala ya kijinsia na kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia na kijamii.
6. Kuchochea na kufanikisha uwezekano wa wanawake kufikia masomo ya kitheologia kuhakikisha uchangamanaji wa wanawake kwenye mafunzo ya kitheologia katika huduma ya kusimikwa ya Kanisa.
7. Kutumia vyombo vya habari kama zana ya kuhimiza na kushughulikia matatizo ya kijinsia.
8. Kuendelea kuwajengea uwezo viongozi chipukizi wanawake wenye malengo maalum.
9. Kuboresha mifumo kwa ajili ya kuendeleza mafunzo miongoni mwa wafanya kazi wanachama kama vile kuwafundisha na kuwalea kuwa na programmu za kuwawezesha wanawake ili waweze kuona haki ya kijinsia kama hitaji la kawaida.
10. Kuhakikisha fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ngazi zote ndani ya muundo wa taasisi.

## *Mpangilio wa kitaasisi*

Jumuiya ya LWF hukazia mtawanyiko na umoja. Hii inamaana kuwa na makusudi katika kuendeleza mipango na kutekeleza mipango kazi ambayo inawawezesha wanawake na kuwezesha ushirikiano kati ya vikundi tofauti kati ya wanawake na wanaume, waliosimikwa na walei, wa umri na tamaduni tofauti - inayopelekea mwelekeo wa mabadiliko ya uongozi shirikishi katika Kanisa na maelezo mengine ya jumuiya.

Utendaji wa ujumuisho unamaana ya kikanisa katika jumuiya: ni jinsi ambavyo Kanisa linataka kuiishi huduma yake ya kinabii ya kubadilisha miundo na mifumo ya ubaguzi kwa kutoa nafasi ya uwazi na upendo kwa watu wote wa Mungu. Utofauti na ujumuisho ni vipengele muhimu katika ushirikiano endelevu ambao huipa umoja wake katika Kristo maamuzi ya baraza yanayothibitisha kuwa hatua zitachukuliwa na mifumo kutengenezwa katika Makanisa ambayo hukumbatia karama ya

wanawake katika uongozi na kukuza ujumuisho katika miundo yote ya kiutawala. Quotas ni miundo ya kimfumo ambayo imeundwa ili kuingilia vikwazo tofauti ya kivitendo ambavyo wanawake mara nyingi hukabiliana nayo kufikia ushiriki sawa kwa misingi ya vigezo sawa.

Hukumbatia ushiriki sawa na uwakilishi sawa kwa wanawake na wanaume katika uongozi ni ishara ya matengenezo ya mabadiliko yanayoendelea katika Kanisa. Kuwasimika wanawake ni ishara moja wapo ya uthibitisho wa kitheologia. Kuwajumuisha wanawake katika huduma ya kusimikwa kusimama kama msingi wa kujenga uraia wa wanawake katika mazingira ya kikanisa na ni hatua moja muhimu ya kutekeleza haki ya wanawake katika maKanisa.

1. Hukuza mabadiliko ya tabia kupitia mijadala na kusaidia jumuia, waumini, na kadhalika.
2. Kuendeleza viwango na mahitaji ya hati ya mshahara sawa kwa jinsia iliyochukuliwa mwaka 2012 katika ofisi ya jumuiya.
3. Kujumuisha ushirikishaji na uwakilishi katika wafanyakazi wa LWF, matukio, mikutano, kamati na vikundi kwa mujibu wa maamuzi ya baraza la 11 kuhusu usawa wa kijinsia.
4. Kuhakikisha sheria ya maadili ya wafanyakazi ya LWF matumizi mabaya ya mamlaka unyonyaji wa kingono unafutwa na wafanyakazi wote bila kukiuka kuendeleza mabadiliko ya sheria ya maadili kati ya Makanisa wanachama na taasisi husika.
5. Kutekeleza ukaguzi wa jinsia kwa ajili ya taasisi zilizopo kwenye jumuiya na taasisi washirika.
6. Kuhakikisha kuwa bajeti ya taasisi, miradi na programmu vyote vina miitikio ya kijinsia.
7. Kuanzisha kundi la wafanya kazi kwenye taasisi watakaoshughulikia masuala ya jinsia(ofisi ya jumuiya, makanisa wanachama /au taasisi wanachama) na majukumu yaliyoelekezwa kusimamia na kuratibu mpango wa sera ya haki ya jinsia.
8. Kuhakikisha ushiriki sawa katika uongozi na taasisi za kufanya maamuzi.

### Maeneo salama na kuponya jumuiya

Kila tendo lenye jeraha linalotokana na ukatili wa kijinsia kwa uumbaji wa sura ya Mungu na linalovunja jumuiya ya waaminio ambao waliitwa katika uhusiano wa haki. Kwa hiyo, ukimya unapaswa kuvunjwa. Jukumu la kinabii la Kanisa ni kutoa mchakato au uponyaji na maeneo salama kwa ajili ya waathirika na wahanga wakishirikiana na wanachama wengineo katika huduma ya uponyaji. Dhamira kamilifu na huduma pia inamaanisha kwamba wahusika wa ukatili wakijinsia wawajibishwe. Hili humaanisha kuwa hata wanaume pia ni sehemu ya mjadala wa kijinsia

wakiangazia jinsi ambavyo vielelezo vya wanaume vinaendeleza ukatili na utawala onevu na ukatili unaotokana na jinsia haijalishi jinsi ambavyo iko sanifu kiutamaduni au linakubalika kwa au vinavyokubalika zaidi vipo katika mazingira tofauti ni uhalifu na ni dhambi: uonevu na ukatili wa kijinsia vinapingana na ukweli wa injili.

Mikakati ya kushughulikia ukatili unaotokana na jinsia kama suala la imani:

1. Kuendeleza utendaji mpya sheria na sera za uma zinazoangazia kujitoa kwa ajili ya haki za jinsia, endapo pale sheria, sera za uma utamaduni au vitendo vya kikanisa havikubaliani na haki ya jinsia au havipo.

2. Kujihusisha na shughuli zinazotoa nafasi salama kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana, kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na ukatili unaotokana na jinsia pamoja na kambi na mazingira ya wakimbizi.

3. Hukuza na kuimarisha mahusiano, mitandao, na uongozi na taasisi zingine za kikanisa taasisi za kijamii na kiraia maajenti wa umoja wa mataifa na serikali pia kuendeleza haki ya kijinsia.

4. Kuchangamanisha mipango iliyoshauriwa katika mpango kazi wa LWF kwa ajili ya Makanisa, "*Makanisa yaseme hapana kwa ukatili dhidi ya wanawake",* kama vile: kuunga mkono kazi za kidiakonia kufafanua zana za kibiblia, kufanya Kanisa kuwa ni mahali salama, kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi za kijamii na taasisi za kiserikali. Na mengine mengi.

### *Mifumo na taratibu za uwajibikaji*

Uwajibikaji wa pande zote mbili na mawasiliano ya wazi huenda bega kwa bega. Pale ambapo programmu na taasisi mara nyingi wanatambua



kwa wazi

uonevu wa kijinsia uwazi wa uwajibikaji hufuata kwa asili. Kujitoa kwa ajili ya uwajibikaji kati ya taasisi zote na watu wote ndani ya jumuiya ya LWF ni muhimu kuhakikisha kwamba vitendo vinalingana na sera kanuni za kitheolojia. Kanuni za uwajibikaji, njia na taratibu vinafikika na ni wazi kwa washiriki wote wa ndani na nje. Uwajibikaji wa pande zote mbili imekitwa katika uhuru wa mkristo kumhudumia jirani yake.

Kila mtu ana hadhi na anastahili haki na uhuru kulingana na tamko la Haki za Binadamu. Kufuatana na haki za binadamu Kanisa limeitwa kuwa sauti kwa ajili ya masikini, walioonewa, waliotengwa, na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Kuwatetea na kutekeleza kuweka katika vitendo sheria za kimataifa za haki ya binadamu ni njia ambayo Makanisa yatafanikisha kujizatiti kwao kwa utu wa mwanadamu na kuwa wakala muhimu wa mabadiliko katika jamii. Haki za binadamu zimetokana na hadhi. Katika nchi ambazo watu wanaishi katika ukatili na mizozo ya kivita, Kanisa linapaswa kutetea, kuheshimu sheria ya kimataifa ya ubinadamu: hili pia hurejea katika ukatili wa kijinsia wa kingono.

Kupuuza na kudharau mahitaji haya tofauti, na haki inaweza kuwa na madhara makubwa sana kwa ajili ya kulinda maisha ya watu wanaokabiliana na dharura au majanga ya kibinadamu. Kuhuisha maswala ya kijinsia kutokana na dharura au majanga ni muhimu kuhakikisha kuwa misaada ya kibinadamu inatolewa na isiwawekewatu katika hali ya hatari bali iwafikie kwa ajili ya kuwaokoa, na huduma hii iwajengee hali ya mtazamo chanya wa hali ya juu.

Mikakati hujumuisha maeneo yafuatayo:

1. Kuibua uelewa kuhusu misada ya kisheria na nyaraka husika za un (tamko la pamoja la haki za binadamu; CEDAW, Yogyakarta maazimio ya Umoja wa Mataifa 1325, mkutano wa Geneva na



# Faharasa

protokali nyongeza): na vyombo vya kikanda kama vile belem do par ā

2. Huendeleza mkabala wa kihaki (RBA) katika maendeleo
3. Kuchukua kanuni za kibinadamu na maadili ya kitabia – mipango inayo endeleza utu wa mwanadamu na/au kuzuia hali zote za unyonyaji wa kingono na matumizi mabaya ya mamlaka na kuhusisha haya yote na muelekeo wa haki ya kijinsia
4. Kuendeleza mafunzo ya dharura yenye muelekeo wa kijinsia
5. Kutumia mkabala wa "Usifanye Madhara" katika kupanga
6. Kutengeneza fursa sawa kwa ajili ya kufikia na kutumia rasilimali katika miradi na mpango.

Jinsia humaanisha tofauti zilizotengenezwa kijamii katika fursa zinazoambatanishwa katika na kuwa mwanamke au mwanaume. Na kwa mchangamano wa kijamii na uhusiano kati ya wanawake na wanaume. Jinsia huamua

kinachotarajiwa, kuruhusiwa na kuthaminiwa katika mwanamke au mwanamume katika mtazamo fulani katika jamii nyingi kuna tofauti na kutokuwiana kati ya wanaume na wanawake katika majukumu na wajibu waliopewa, shughuli zinazofanyika, kumiliki na kusimamia rasilimali, vilevile na katika fursa za kufanyia maamuzi.

Uchambuzi wa jinsia ni zana ya kuelewa tofauti kati ya tofauti iliyopo baina ya ukweli wa wanawake na wanaume. Katika mtazamo wowote. Inatambulika kuwa swala hilohilo huwaathiri wanawake na wanaume kwa namna tofauti na pasipo uwiano na kuchangamotisha dhana kuwa kila mtu anaathiriwa na jambo fulani kwa namna hiyohiyo. Pasipo kujali mtazamo wao

uwiano wa kijinsia inamaanisha usawa wa uwakilishi na ushiriki wa wanaume na wanawake.

Takwimu zenye ubaguzi wa kijinsia : thamani ya uchambuzi wa takwimu za taarifa yenye ubaguzi wa kijinsia[12]

Takwimu zenye ubaguzi wa jinsi na jinsia zimechanganywa pamoja:

Ukusanyaji na utofautishwaji wa taarifa za takwimu na data kwa jinsia kuwezesha

---

**12**

**www.actalliance.org/resources/policies-and-uidelines/gender/ACT%20Gender%20Policy%20approved%20by%20GB%2006%20Sept%202010.pdf**

ulinganisho katika uchambuzi wa kijinsia. data zilizokusanywa na kuchambuliwa kwa mfululizo ili kuelewa athari za muitikio wa kibinadamu katika wakazi wote wa eneo husika. [13]

Uwiano wa kijinsia inamaana fursa sawa, haki na wajibu kwa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana. Usawa hauna maana kwamba wanaume na wanawake wamefanana bali fursa za wanawake na wanaume haki na wajibu hautegemei labda kwamba wamezaliwa mwanamke au mwanaume. Inamaanisha kwamba mapendeleo mahitaji na vipaumbele vya wanaume na wanawake vinazingatiwa.

Inaonyesha kuwa jinsia ni namna ambayo usawa wa kijinsia unafikiwa. Inamaanisha kuwahudumia kwa usawa wanawake, wasichana, na waume kwa mujibu wa mahitaji yao maalum na mtazamo wao maalum.

---

[13] Ibid

Kuhakikisha haki hatua lazima zipatikane za kufidia manufaa ya kihistoria na kijamii ambayo huwazuia wanawake na wanaume kutokana na

kufanya kazi katika uwanja sawa wa michezo.[14]

Utambulisho wa jinsia humaanisha utambulisho binafsi na mtazamo alionao mtu kuhusu yeye na uhuru wa kujieleza. Ni kuhusu nini maana ya kuwa mvulana au

kuwa msichana, mwanaume au mwanamke pia ni sifa zote na tabia ambazo utamaduni wetu hutarajia jinsia moja wapo awenazo. [15]

Haki ya kijinsia huonyesha Ulinzi na ukuzaji wa utu wa mwanamke na mwanaume ambae, aliumbwa kwa mfano wa Mungu na ni wakili mwajibikaji mwenza kwa uombaji. Haki ya kijinsia. Kudhihirishwa kupitia usawa na uwiano katika uhusiano wa mamlaka kati ya wanawake na wanaume na utokomezaji wa mifumo binafsi manufaa na uonevu wa taasisi. Utamaduni na mifumo binafsi ambayo huendeleza ukandamizaji.

[14] Ibid

[15] Ibid

Uchambuzi wa jinsia: uchambuzi wa kijinsia ni mchakato wa kushughulikia mambo ya kijinsia kutoka mwanzo haki mwisho wa mkakati wowote uliopangwa.

> Ni mkakati wa kuwafanaya wanawake na wanaume pia wahusike na kuzoelea mipaka ya ubunifu na utekelezaji usimamizi na tathimini ya sera na mipango katika maendeleo
> yote ya kisiasa kiuchumi na kijamii ili kwamba wanawake waweze kunufaika kwa usawa na uonevu hauendelezwi. Lengo la mwisho ni kufikia Usawa wa mwisho. (Imekitwa kwenye baraza la umoja wa mataifa uchumi na jamii ECOSOC). [16]

Unyeti wa kijinsia: uelewa sawa wa mahitaji wajibu na majukumu tofauti ya wanawake na wanaume katika muundo tekelezaji usimamizi na tathimini ya sera na mipango katika maeneo yote[17].

Jinsi inamaanisha tofauti za kibaiolojia baina ya wanawake na wanaume tofauti za kijinsia ni kuhusu miili ya wanaume na wanawake na kazi zao za kibaolojia.[18]

[16] At **www.un.org/womenwatch/osagi/intergovernmentalmandates.htm**

[17] Act Alliance, op. cit. (note 12).

Data zenye ubaguzi wa kijinsia. Takwimu au taarifa za kitarakimu juu ya tofauti kati ya wanaume, wanawake, wavulana na wasichana[19]

Uwezeshwaji wa wanawake ni mchakato wakubadilisha mamlaka ya

kijinsia katika mahusiano, kuendeleza ufahamu wa utii wa wanawake na kujenga uwezo wao kwa ujumla katika kuichangamotisha. Kwa ajili ya sababu za kihistoria za kutengwa na kubaguliwa, kama mkazo katika kazi ya wanawake katika maendeleo bado ni muhimu katika kuunga mkono juhudi za kufikia haki binafsi au ya ujumla ya wanawake kushiriki kama mawakala waliowezeshwa kikamilifu wa mabadiliko katika Kanisa na jamii. Mchakato hukazia ngazi ya binafsi kwa kuwasaidia wanawake kukuza ujasiri binafsi.ni kipengele muhimu katika kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika michakato ya kufanya maamuzi. Kuwajumuisha na kuwawezesha wanawake ni muhimu ili kwamba kuunda jumuiya endelevu, makanisa na jamii. Kuboresha hadhi ya wanawake kufanikisha uwezo wao wakufanya maamuzi na uongozi katika ngazi zote na katika maeneo yote ya maisha.

[18] Ibid

[19] Ibid

# Msaada katika mtandao wa kujifunza sera ya kijinsia

*ACT*
www.actalliance.org/resources/policies-and-guidelines/gender/ACT%20Gender%20Policy%20approved%20by%20GB%2006%20Sept%202010.pdf/view

*APRODEV*
www.aprodev.eu/index.php?option=com_content&view=article&id=69&Itemid=29&lang=en

*CARE International*
http://gender.care2share.wikispaces.net/CARE+International+Gender+Policy

*International Federation of Red Cross and Red Crescent Societies (ICRC):*
www.ifrc.org/Global/Governance/Policies/gender-policy-en.pdf

*International Labour Organisation (ILO)*
www.ilo.org/public/english/region/asro/mdtmanila/training/unit1/harvrdfw.htm

*National Council of the Churches of Christ in the USA (NCCC)*
www.ncccusa.org/pdfs/gender-4web.pdf

*UN Habitat*
http://ww2.unhabitat.org/pubs/genderpolicy/role.htm

*United Nations Development Programme (UNDP)*
http://hrba.undp.sk/index.php/assessment-analysis-and-planning/gender-assessment/genderchecklist

*World Health Organisation (WHO)*
www.who.int/entity/gender/mainstreaming/Gender_Manual_Glossary.Pdf


THE
LUTHERAN
WORLD
FEDERATION
A Communion
of Churches